

**KUCHUNGUZA MCHOMOZO KATIKA FASIHI YA KISWAHILI:  
UTAFITI LINGANISHI WA USHAIRI KATIKA DIWANI YA USTADHI  
ANDANENGA**

**AUGUSTINO TENDWA**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SHARTI  
PEKEE LA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA  
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2017**

**UTHIBITISHO**

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma tasinifu hii iitwayo:  
*“Kuchunguza Mchomozo katika Diwani ya Amir Sudi Andanenga”*, na nimeridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa kwa ajili ya Utahini wa Shahada ya Uzamili ya Fasihi kwa Kiswahili (M.A. Kiswahili-Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

**Dkt. Profesa Tigiti .S.Y.Sengo**

**(Msimamizi)**

.....

Tarehe

### **HAKIMILIKI**

Tasnifu hii au sehemu yake yoyote hairuhusiwi kukaririwa, kuhifadhiwa, Kubadilishwa au kuhaulishwa kwa mbinu yoyote ile: kielektroniki, kimekanika, kunakilishwa, kurudufiwa, kupigwa picha, au kurekodiwa kwa utaratibu wowote ule katika hali yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba yake.

**TAMKO**

Mimi, John Augustino Tendwa, nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Shahada yoyote.

.....  
Saini

.....  
Tarehe

**TABARUKU**

Natabaruku kazi hii kwa watoto wetu wapendwa Juliety Tendwa na Oliver Tenda,  
pia bila ya kuwasahau wataalamu na wanafunzi wote wa fasihi ya Kiswahili.

## SHUKRANI

Katika mafanikio yoyote, upo mchango wa kimawazo, kifedha ama kiutendaji na kwa sababu mafanikio ya kazi hii sikuweza kujitegemea mwenyewe kwa kila kitu, inanipasa kutoa shukrani zangu za pekee kwa watu ama taasisi zilizofanikisha katika malengo yangu. Nikianza na shukrani za pekee kwa yeye anayetupatia pumzi ya uhai na kutupatia riziki kubwa kubwa na ndogo ndogo ambaye ni Mwenyezi Mungu kwani katika mafanikio haya si kwa nguvu zangu bali ni kwa neema yake. Wapo watu ambao inanipasa kuwafanyia iliyo haki kwa kuwataja katika kufanikisha katika tasnifu hii; shukrani za pekee kwa mwalimu na Msimamizi wangu Dkt, Profesa T.S.Y .Sengo kwa juhudi zake alizonifanyia kwa kusimamia na kuisahihisha kazi hii hadi kufikia ubora huu, hakika anapaswa kuheshimiwa kwa mchango wake na anastahili kuigwa kwa mazuri haya. Naweza kumbuka maneno yake ya kutia moyo ambayo mara nyingi alikuwa akiyatumia, ‘tusichoke’ neno hilo lilikuwa likinitia moyo sana kwani alikuwa ananiambia mara nyingi kuwa ukiwa na mimi hauwezi choka. Mengi yaliyo katika kazi hii ni sehemu tu ya matunda ya ujuzi wake mkubwa na ushauri wake wa kitaalamu. Ninapenda pia kumshukuru Prof. Emmanuel Mbogo na Prof.T.S.Y Sengo kwa kunifanikisha katika kukamilisha tasnifu hii, kwani amekuwa akinitia moyo na kutoa muda wake mwingi kunielekeza kwani mara nyingi nilitaka kufahamu undani wa kazi yake ya tamthiliya ambayo nimeitumia katika kazi hii. Siwezi kumsahau Msanii wa kazi za kifasihi nilizozitumia katika tasnifu hii, *Nyerere na safari ya Kanaani na Wangari Maathai* [Amri A. Andandanenga] kwani alikubali kutusaidia kununua na kutuuzia nakala moja kutoka kwa mchapishaji, naomba Mwenyezi Mungu ambariki sana.

**IKISIRI**

Lengo la utafiti huu kama lilivyobainishwa katika sura ya kwanza ilikuwa ni kuchunguza Mchomozo katika Diwani ya Ustadh Andanenga ili kubaini vipengele vya Mchomozovilivyotumika katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Utafiti huu ulitumia mbinu moja ya ukusanyaji data ambayo ni; maktaba. Aidha data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi linganishi. Utafiti huu uliongozwa na *Nadharia ya Karl Maks* katika Uchambuzi wa Matini za Kifasihi. Utafiti umegundua kuwa, *Diwani ya Ustadh Andanenga* imetumia vipengele vya mchomozo ambavyo ni takriri na ukengeushi. Aidha utafiti huu umebaini kuwa, kipengele cha takriri silabi / mizani ndicho kimejitokza zaidi. Utafiti huu umebaini kuwa diwani hii iliandikwa katika cha mwaka 1990, msanii akiwataka wananchi kufanya kazi na kujitegemea ili kuepuka kutegemea misaada kwa Wazungu. Diwani inawataka watu waishi kwa kupendana, wathamini lugha ya Kiswahili kwani huo ni ukombozi wa kifikra endapo tutathamini utamaduni wetu.

## YALIYOMO

<b>UTHIBITISHO</b> .....	ii
<b>HAKIMILIKI</b> .....	iii
<b>TAMKO</b> .....	iv
<b>TABARUKU</b> .....	v
<b>SHUKRANI</b> .....	vi
<b>IKISIRI</b> .....	vii
<b>JEDWALI</b> .....	xi
<b>KIELELEZO</b> .....	xii
<b>SURA YA KWANZA</b> .....	1
<b>1.0 UTANGULIZI</b> .....	1
1.1 Utangulizi .....	1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .....	2
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti .....	5
1.4 Malengo ya Utafiti .....	5
1.4.1 Lengo Kuu .....	5
1.4.2 Madhumuni ya Utafiti .....	6
1.5 Maswali ya Utafiti .....	6
1.6 Umuhimu wa Utafiti .....	6
1.7 Mipaka ya Utafiti .....	7
1.8 Matatizo ya Utafiti .....	7
1.9 Mpangilio wa Tasnifu .....	8
1.10 Hitimisho .....	8



<b>SURA YA PILI</b> .....	9
<b>2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA</b> .....	9
2.1 Utangulizi .....	9
2.2 Dhana ya Ushairi .....	9
2.3 Dhana ya Fasihi Linganishi.....	11
2.4 Mchomozo.....	13
2.4.1 Aina za Mchomozo.....	14
2.4.2 Mchomozo Ukengeushi/ Ukiushi .....	17
2.5 Maudhui .....	17
2.5.1 Ujumbe.....	18
2.6 Pengo la Maarifa.....	19
2.7 Dhana ya Nadharia .....	19
2.8 Kiunzi cha Nadharia .....	20
2.9 Nadharia ya Umaksi ( Marxist theory) .....	21
2.9.1 Sifa Za Uhakiki wa Kimarx .....	23
2.10 Hitimisho.....	23
<b>SURA YA TATU</b> .....	25
<b>3.0 MBINU ZA UTAFITI</b> .....	25
3.1 Utangulizi .....	25
3.2 Eneo la Utafiti.....	25
3.3 Mbinu ya Usomaji wa Maktabani .....	26
3.3.1 Matini.....	26
3.2.2 Uchambuzi wa Data.....	27

3.3	Hitimisho.....	27
	<b>SURA YA NNE</b> .....	29
<b>4.0</b>	<b>UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA</b> .....	29
4.1	Utangulizi.....	29
4.2	Uteuzi na Matumizi ya Vipengele vya Mchomozo .....	29
4.2.1	Mchomozo katika Diwani ya Ustadh Andanenga .....	30
4.2.2	Mchomozo Ukengeushi/ Ukiushi .....	58
4.3	Kulinganua na Kulinganisha Uteuzi wa Mbinu za Mchomozo katika Diwani ya Ustadh Andanenga .....	61
4.3.1	Kutofautiana .....	62
4.3.2	Kufanana .....	63
4.4	Sababu za Kufanana Na Kutokufanana .....	63
4.5	Hitimisho.....	64
	<b>SURA YA TANO</b> .....	65
<b>4.0</b>	<b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO</b> .....	65
5.1	Utangulizi.....	65
5.2	Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti.....	65
5.3	Hitimisho.....	69
5.4	Mapendekezo.....	70
	<b>MAREJELEO</b> .....	72
	<b>VIAMBATISHO</b> .....	77

**JEDWALI**

Jedwali Na 4.1: Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Mchomozo kwa  
ujumla .....61

**KIELELEZO**

Kielelezo: Na 2.1: Uhusiano baina ya vipengele vya Mchomozo.....17

## **SURA YA KWANZA**

### **1.0 UTANGULIZI**

#### **1.1 Utangulizi**

Sura hii ni sura tangulizi ambayo imetoa usuli wa tasnifu hii. Katika kubainisha usuli wa tatizo na tatizo lililofanyiwa utafiti. Sura hii inahusu usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na hitimisho.

Kabla ya kuanza tupate historia fupi ya mtunzi wa Diwani ya Ustadh Andanenga. Amiri Abdalah Sudi maarufu kwa jina la kishairi Andanenga, alizaliwa tarehe 02 Oktoba, 1963, huko Kilwa. Mwaka 1949 alipelekwa shule ya msingi Kikole huko Kilwa. Baada ya kufaulu mtihani wa darasa la nane huko Mtanga, alichaguliwa kujiunga na shule ya sekondari ya Songea. Hakuendelea na masomo, alikomea kitado cha pili. Ni mshairi hodari na makini katika utenzi wa malumbano. Ni mwimbaji. Ikitambua hilo BAKITA iliwahi kumuomba kuimba utenzi wa INKISHAFI. Kabla ya kuugua macho na kupofuka aliwahi kuwa mtumishi katika idara na Wizara serikalini hadi mwaka 1975. Tumeamua kufanya utafiti katika Diwani ya Ustadh Andanenda kutokana na kwamba mshairi huyu aliwahi kufahamika sana katika siku za nyuma kutokana uimbaji wake wa mashairi redioni wakati akiwa mgonjwa wa macho asiyeona (kipofu). Hivyo, mtafiti alivyutiwa na kuona haja ya kuangalia na kuchunguza mchomozo na vipengele vyake kama moja wapo ya ushairi wa kimapokeo na ule wa kisasa. Andanenga ni Mtanzania, hivyo tatizo la baadhi ya wasomi kudharau matumizi ya lugha ya Kiswahili anayafahamu kwa ukaribu. Tatizo

ukoloni mamboleo na watu kutegemea misaada zaidi analifahamu. Diwani yake imesheni changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili raia wa nchi ya Tanzania.

## **1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Dhana ya ushairi kama ilivyofasiliwa na Wamitila (2010:226), Ushairi ni utungo wa sanaa ya lugha na mpangilio maalum wa mishororo au wa kisauti na kwa maneno mateule kwa kutumia mbinu za lugha zenye mnato na mbinu nyinginezo za kibalagha na kimtindo zinazomwezesha mtunzi kuwasilisha ujumbe kwa ufupi na kwa mkokotezo mkubwa unaoeleza kisa, hisia, tukio au hali kwa lugha ya mkato. Uzito hasa wa shairi upo kwenye uwezo wake wa kuzigusa hisia na mkuruba au uhusiano wake wa karibu na muziki.

Kazi ya fasihi ina vipengele vya kifani ambavyo hutumiwa na wasanii wa kazi za fasihi katika kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Matumizi ya vipengele hivyo hutegemea tajiriba ya mtunzi wa kazi ya fasihi, wakati na muktadha maalumu. Hivyo katika kuchambua matini yoyote ya fasihi, mchambuzi hana budi kuvifahamu vipengele vya fani ambavyo ndivyo hubeba maana ya matini. Mbali na fani ambayo hubeba maudhui ni vema kwa mchambuzi wa matini kuifahamu historia ya mtunzi, kipindi kile ambapo msanii aliishi na wakati ule ambao kazi ya fasihi ilitungwa. Senkoro (2011) na Wamitila (2003) wote wanakubaliana kwamba, mtunzi wa kazi ya fasihi ili aweze kutunga kazi yoyote hawezi kukwepa suala la kuifahamu historia ya jamii husika anayoandikia, kwani kama hataifahamu jamii yake vizuri kuna hatari kazi yake ikawa imepitwa na wakati kabla hata ya kuikamilisha. Vile vile hata yule mhakiki na mchambuzi wa matini hanabudi kuifahamu vizuri historia ya jamii yake,

hasa wakati ule kazi husika iliandikwa na historia ile ya msanii wake ili aweze kujua vizuri kile ambacho msanii wake alikilenga. Kwani mhakiki asipojua vizuri historia ya jamii husika hatakuwa na uwezo mzuri wa kubainisha maudhui hasa yaliyokusudiwa na msanii huyo. Historia ni vipindi tofauti tofauti ambavyo hujitokeza katika jamii na kila msanii wa kazi ya fasihi, huishi katika jamii mbali mbali na katika kipindi tofauti cha historia tofauti. Hivyo ujumbe wowote uliomo katika kazi ya fasihi umebainishwa vizuri na mhakiki kwa kuzingatia; historia ya jamii husika, kipindi ambapo msanii aliishi, mfumo wa maisha na muktadha husika wa uandishi wa kazi hiyo ya fasihi.

Hivyo basi, tunapochunguza ama kuchambua ujumbe wa kazi za kifasihi hatuwezi kuepuka vipengele vya kintindo vya kazi hizo. Kama anavyoeleza Leech (1969) kazi ya fasihi haiwezi kueleweka vizuri bila kuwa na maarifa ya lugha ambayo ndiyo njia ya kujieleza. Kwa hiyo, ili kuelewa kazi ya fasihi ni lazima kuchunguza nduni za kiisimu za lugha fulani na jinsi msanii anavyozitumia kwa kuzihusianisha na malighafi za kiisimu ili kuelewa kile kinachowasilishwa. Hilo tunakubaliana nalo, na katika kazi yetu ni kichunguza kipengele cha mchomozo ambacho ni kipengele katika mtindo.

Kipengele cha Mchomozo kitatusaiadia kubainisha maana ya matini katika kazi ya fasihi. Hivyo utafiti huu utajikita kuchunguza kipengele cha Mchomozo kilivyotumiwa katika *Diwani ya Ustadhi Andanenga* iliyoandikwa na Amir A. Sudi Andanenga. Lengo hasa ni kuchunguza jinsi msanii wa diwani hiyo alivyoweza, kutumia kipengele cha mchomozo katika kufikisha maudhui yake kwa jamii.

Katika kazi ya fasihi, si rahisi kupata ujumbe bila kuangalia mtindo. Mtindo una vipengele vya mchomozo ambavyo hutumiwa na wasanii kuwasilisha ujumbe wa kazi za sanaa. Imeelezwa na baadhi ya watafiti kuwa maana ya kazi ya fasihi hujikita katika vipengele vya lugha kama vile sitiari, tashibiha, tashihisi, kejeli, methali, misemo na nahau (Mutembei, 2002; Mosha, 2002; Wamitila, 2003; Jilala, 2008 & 2010; Senkoro, 2011). Hivyo basi, utafiti huu haukuchunguza kipengele cha lugha yote, badala yake umechunguza vipengele vya mchomozo ili kubaini ni namna gani msanii wa mashairi ya *Diwani ya Ustadhi Andanenga* alivyotumia vipengele vya Mchomozo katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii husika.

Kwa maana hiyo basi, utafiti huu ni utafiti linganishi ambao umelenga kuchunguza vipengele vya mchomozo na dhima yake katika kufikisha ujumbe kwa jamii husika kwa kutumia *Diwani ya Ustadh Andanenga*, iliyoandikwa na Amir.A Sudi Andanenga.

Katika fasihi linganishi, mlinganishi ameweza kulinganisha vipengele vya mchomozo ambavyo vimefikisha maana ya matini kwa kila shairi na kwa diwani yote

Utafiti huu umeangalia suala la kihistoria ambapo katika jamii yoyote ile lazima ipitie vipindi mbalimbali vyenye kutengeneza historia ya jamii husika, ni dhahiri kuwa kuna mchango mkubwa sana wa historia katika kazi za kifasihi kwani husaidia kizazi kilichopo na kijacho kufahamu wapi jamii inakotoka, mahali ilipo na mahali inapoelekea, ambapo yale yanayoonekana kutofaa hukemewa na kuwa mfano wa



yale yasiyohitajika na yale ambayo katika historia yanafaa huendelezwa ili kuijenga jamii. Katika kazi za kisanaa huwezesha kuona namna wasanii waliopita walivyosanii kazi hizo na kipi cha kuboresha na kipi kinabaki kama historia. Kulingana na hoja hizo utafiti huu uliona ni vyema kuchunguza vipengele vya kimaudhui katika kudhihirisha mchango wa historia katika ukuaji wa tamthiliya ya kiswahili.

### **1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti**

Waandishi wa kazi za fasihi wanaweza kuelezea suala moja katika jamii kwa kutumia vipengele mbali mbali vya mchomozo. Waandishi wanaweza kuwa wawili au zaidi na wakaongelea suala lile lile, lakini wakatofautiana namna ambavyo kila mmoja anavyowasilisha ujumbe wake kwa jamii. Hivyo basi bado kuna haja ya kujua kuwa mwandishi wa kazi ya ushairi mmoja alitumiaje kipengele vya mchomozo katika diwani yake. Utumiaji huo wa kipengele cha Mchomozo kimetumiwaje na dhima yake ni ipi . Hivyo basi tatizo la utafiti ni kuangalia jinsi, mwandishi mmoja wa ushairi alivyoweza kutumia mbinu ya Mchomozo katika kuwasilisha kazi yake.

### **1.4 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahsusi kama ifuatavyo:

#### **1.4.1 Lengo Kuu**

Utafiti huu ulichunguza vipengele vya mchomozo na dhima ya vipengele hivyo katika kufikisha maana ya matini, katika ushairi wa *diwani ya Ustadh Andanenga*.

### 1.4.2 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu una madhumuni matatu:

- i) Kubainisha vipengele vya Mchomozo katika diwani ya *Ustadh Andanenga*.
- ii) Kubainisha tofauti na kufanana kwa vipengele vya mchomozo.
- iii) Kubainisha sababu za kufanana na kutofautiana huko.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unajibu maswali yafuatayo:

- i) Ni vipengele vipi vya Mchomozo vilivyojitokeza katika *diwani ya Ustadh Andanenga?*
- ii) Ni aina ipi ya Mchomozo iliyojitokeza zaidi katika diwani ya *Ustadh Andanenga?*
- iii) Sababu za kutofautiana huko ni zipi?

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa utafiti huu umejikita katika nyanja kuu tatu; kwanza, matokeo ya utafiti huu yataongeza maarifa katika nadharia na mbinu za utunzi wa ushairi hususani ushairi wa Kiswahili. Pili, utafiti huu utatoa mchango katika maarifa ya taaluma ya fasihi linganishi nadharia na mbinu. Hivyo basi, utafiti huu utaweza kutumiwa kama marejeo, hususani katika fasihi linganishi. Kwa maana hiyo, utawasaidia wanafunzi na watafiti wengine kupata marejeo kuhusu fasihi linganishi na tamthiliya ya Kiswahili kwa ujumla wake. Tatu, utafiti huu pia utakuwa ni changamoto kwa watafiti wengine kufanya utafiti kuhusu mbinu ya mchomozo katika ushairi wa Kiswahili na vilevile utatajirisha maktaba ya chuo.

### **1.7 Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu unalenga kuchunguza vipengele vya mchomozo vilivyotumiwa na mwandishi katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Zipo diwani nyingi kama vile diwani ya Mathias Mnyampala, diwani ya Midilu ya Tigiti Sengo, diwani ya Charles Mloka, Mashairi ya Chekacheka, mashairi ya Saadan Kandoro na mengine mengi. Lakini utafiti huu utajikita peke yake katika kutachambua mchomozo tu katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*.

Aidha, mchomozo una vipengele vingi vinavyotumika katika kufikisha ujumbe wa fasihi, utafiti huu haukulenga kuchunguza vipengele vyote vya mchomozo, bali ulijikita katika kuchunguza kwa kina vipengele vichache vya mchomozo ambavyo ni mchomozo takriri na ukengeushi kwa undani. Mtafiti ameamua kufanya hivi, kutokana na kwamba, ujumbe ambao tumeupata katika kuchunguza vipengele vya takriri na ukengeushi, ndio huo pia, tungepata kwa kuongeza kipengele cha mchomozo usambamba. Na, dhana ya usambamba inafanana kwa ukaribu na dhana ya takriri.

### **1.8 Matatizo ya Utafiti**

Katika utafiti huu, mtafiti alikutana na matatizo kadhaa ambayo yameifanya kazi ya kiutafiti kuwa ngumu, ila alijitahidi kuyatatua. Mojawapo ya tatizo kubwa lilikuwa upatikanaji wa kitabu cha *Diwani ya Ustadh Andanenga*, kitabu hiki imekuwa ni vigumu kukipata maana ni diwani ya zamani ambayo kwa sasa haipatikani katika maduka ya vitabu. Kuipata diwani hii mtafiti alilazimika kwenda kumtafuta mtunzi mwenyewe kwake Kinondoni mtaa wa Manyanya na kumpatia kiasi cha pesa

ambacho mtunzi naye alikwenda kuinunua nakala moja kwa mchapaji, na hivyo kupata nakala moja ambayo tumeitumia katika utafiti huu.

Tatizo la pili, ni upatikanaji wa pesa. Kazi zote za kitafiti zitahitaji fedha za kutosha, hivyo mtafiti alilazimika kukopa fedha katika benki ili kukamilisha utafiti huu. Tatizo la tatu, diwani hii ni yazamani kidogo, hivyo hatukuweza kupata uchambuzi wake ambao ungekuwa msaada katika utafiti wetu.

### **1.9 Mpangilio wa Tasnifu**

Muundo wa tasnifu hii umegawanyika katika katika sura tano, sura ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla wa utafiti, masuala yanayohusiana na tatizo lililofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu, yamejadiliwa na kutolewa maelezo ya kina. Sura ya pili inahusu utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia, ambapo sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti. Katika sura hii, tumeonesha mbinu za ukusanyaji data, mbinu za uteuzi wa sampuli na kujadili mkabala uliotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Sura ya nne, inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data na sura ya tano, ambayo ndiyo sura ya mwisho, inahusu muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo.

### **1.10 Hitimisho**

Sura hii imejadili juu ya usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa tasnifu. Aidha katika sura hii ya kwanza tatizo la utafiti litakuwa limebainishwa na kuelezwa wazi na kwa undani zaidi. Sura inayofuata ni sura ya pili, ambayo inahusu mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha Nadharia.

## SURA YA PILI

### 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

#### 2.1 Utangulizi

Sura hii inatalii mapitio ya maandiko tangulizi. Katika sura hii maandiko na tafiti mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti zimejadiliwa kwa kina na hatimaye kuibua pengo la maarifa ambalo liliweka msukumo kufanya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne ambapo sehemu ya kwanza inahusu dhana ya fasihi linganishi, sehemu ya pili inajadili juu ya vipengele vya maudhui, ya tatu ni pengo la kimaarifa na sehemu ya nne kiunzi cha nadharia.

#### 2.2 Dhana ya Ushairi

Ushairi ni utanzu mmoja wapo katika fasihi ya Kiswahili. Utanzu huu umetolewa fasili mbalimbali na wataalamu wengi. Baadhi yao ni hawa na maelezo yao juu ya ushairi.

Shaaban (1958), anaeleza kuwa,

*Ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na utenzi. Zaidi ya kuwa sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari...Mawazo, maono na fikra za ndani zinapoelezwa kwa muhtasari wa Ushairi huvuta moyo kwa namna ya ajabu.*

Katika maelezo hayo ya Shaaban tunapata zaidi hisia yenye kugusa mioyo wakati mtu anaposikiliza ushairi. Na, maelezo hayo yanaungwa mkono na Abed (1954:1), Mnyampala (1965) na Mayoka (1986). Wao wamejikita zaidi kwa kuonyesha kuwa Ushairi ni wimbo, wenye maneno ya hekima, lugha ya mkato, lugha nzito, urari wa mizani na vina, pamoja na hisia (wenye kuvuta moyo). Katika utafiti wetu huu

tunakubaliana na maelezo yaliyotolewa na Wanazuoni hao, kwani Ushairi ni vizuri kuwa na kanuni, taratibu na ulete hisia kwa msikilizaji na msomaji wa kazi ya Ushairi.

Hata hivyo, Mulokozi na Kahigi (1982:25) wanaeleza kuwa,

*Ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilo maalumu wa maneno fasaha na yenye muwala, yaliyoandikwa kwa lugha ya mkato, picha, sitiari au ishara, katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo, ili kuleta wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisia fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo.*

Kwa mfano, Massamba akimunukuu Shaababn Robert , anaungana nao naye na wengine Massamba (1983:55), anaeleza kuwa,

*Ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi, tenzi. Zaidi ya kuwa sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari. Mwauliza wimbo. Shairi na tenzi ni nini? Wimbo ni shairi ndogo, ushairi ni wimbo mkubwa na utenzi ni upeo wa ushairi. Mwauliza tena kina na ufasaha huweza kuwa nini? Kina ni mlingano wa sauti za herufi. Kwa maneno mengine huitwa mizani ya sauti, na ufasaha ni uzuri wa lugha. Mawazo maono na fikra za ndani zinapoelezwa kwa muhtasari wa shairi huvuta moyo kwa namna ya ajabu.*

Abdailatif Abdalla akiniukuliwa na Massamba 1983: 57), naye anaeleza kuwa,

*Utungo ufaao kupewa jina la ushairi si utungo wowote bali ni utungo ambao katika kila ubeti wake kuna ulinanifu wa vina vitukufu vilivyopangwa kimoja baada ya chenziye, wenye vipande vilivyo na ulinganifu wa mizani zisizo pungufu wa zisizo zaidi. Na vipande hivyo view vimetandwa na maneno ya mkato maalum na yenye lugha nyoofu, tamu na lainai. Lugha ambayo uzito wa fikra, tamu kwa mdomo wa kusema, tumbuizi kwa masikio ya kuusikia na yenye kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ilivyokusudiwa.*

Katika utafiti huu , tumekubaliana na maelezo juu ya Ushairi unaozingatia urari wa vina, mizani, mpangilio maalumu wa maneno, lugha muwala, lugha ya mkato na

wenye kufuata taratibu na kanuni ambazo hutambulisha ushairi wa Kiswahili. Mwandishi wa *Diwani ya Ustadh Andanenga* ametumia sifa za Ushairi wa Kiswahili katika kutunga kazi yake. Hivyo, utafiti huu unaliweka wazi hilo pia juu ya sifa za *diwani ya Ustadh Andanenga*.

### **2.3 Dhana ya Fasihi Linganishi**

Guyard (1964) anasema kuwa, Fasihi linganishi ni tawi la historia ya fasihi ambapo anadai ni somo la mahusiano, mapatano, na maelewano ya kimataifa baina ya kazi na maisha ya waandishi wanaotoka katika fasihi tofauti. Wellek (1988) anaifasili fasihi linganishi kuwa ni somo linalojishughulisha na uhusiano wa vitu viwili ambapo vinaweza kuwa kazi ya mtu binafsi, waandishi au kundi la waandishi na binadamu au fasihi kwa ujumla. Kwa upande wake, Wellek (1988) anaiona fasihi linganishi kuwa ni somo la fasihi nje ya mipaka ya nchi moja, ni kujifunza uhusiano baina ya fasihi kwa upande mmoja na eneo lingine la maarifa mfano sanaa, falsafa, historia ya sanaa za jamii, sayansi, dini na mambo mbalimbali ya kijamii. Wellek na Warren (1996) wanaielezea fasihi linganishi kuwa ni mbinu itumiwayo na wahakiki wengi wa fasihi hata wanasayansi kujadili njia maalum ya usomaji wa sanaa mbalimbali ulimwenguni. Wanakubaliana kuwa ni taaluma inayoshughulikia tofauti au kufanana kwa fasihi ya makundi mawili au zaidi ya kiisimu, kiutamaduni, kihistoria, kiitikadi, kiuchumi, kijamii na kimataifa, japokuwa fasihi linganishi inatumika kulinganisha kazi za fasihi za lugha tofauti. Mfano, Kijerumani, kichina, Kiingereza, Kiswahili na nyinginezo, lakini bado inajishughulisha na fasihi ya lugha moja ikiwa kazi hizo asili yake ni nchi tofauti au utamaduni na vipindi tofauti ndani ya lugha hiyo. Wamitila (2003) anaeleza kuwa fasihi linganishi inahusu uchambuzi wa maandishi ya wakati

mmoja na aina moja na katika lugha mbali mbali kwa nia ya kumiliki sifa zinazoyahusisha kama athari, vyanzo, sifa zinazofanana ama kutofautiana za kiutamaduni.

Hivyo tunaweza kusema kuwa fasihi linganishi inajikita zaidi kutumia mbinu za kiulinganishi baina ya kazi mbili za fasihi ili kujua sifa fulani fulani kama vile kufanana kwa kazi hizo au kutofautiana, tofauti zaweza kuwa za kiutamaduni au za kimazingira.

Jilala (2016), anatumkumbusha kwamba;

*“Fasihi linganishi si tofauti na fasihi kwa vile zote ni taaluma zenye kutumia nadharia na mbinu tofauti katika uwasilishaji na matumizi yake”. Pia fasihi linganishi ni taaluma inayojitegemea, yenye nadharia zake na ambazo ndiyo msingi wa maarifa ya utendaji wake.*

Fasihi linganishi katika utafiti huu imetusaidia kuweza kuweka mipaka ya kiulinganishi na pia kujua taaluma ya fasihi linganishi ambayo ndiyo hasa utafiti huu umekusudia kufanya. Pia fasihi linganishi imetusaidia kujua ni namna gani tunaweza kufanya ulinganishaji wa kazi za fasihi na vipengele vipi vya kuzingatia katika ulinganishaji wa kazi za fasihi katika jamii yetu. Jilala (2016) anasema, fasihi linganishi inatusaidia kubainisha, kutofautisha, kufanana na kuhusiana kwa fasihi za ulimwenguni, itikadi na mielekeo ya jamii tofauti. Kwa mfano, kwa kutumia fasihi linganishi tunaweza kubaini tofauti za kiutamaduni na kifalsafa za jamii ya Kiswahili. Hivyo katika kazi ya utafiti huu linganishi, utatusaidia kutambua m audhui mbali mbali ambayo yamebainishwa katika jamii ya Watanzania.



Katika kazi yetu ya utafiti tunaangalia mchango wavipengele vya mchomozo vinavyotumika katika kutoa mchango wa maudhui katika jamii yetu.

#### **2.4 Mchomozo**

Dhana ya mchomozo imefasiliwa na kuelezwa na wataalamu mbali mbali kama ifuatavyo: Jilala (2016) anasema, hii ni hali ya kuwa na maneno au dhana zinazojitokeza ama kusikika zaidi ya nyingine katika kazi ya fasihi. Ujitokezaji huu huwa ni wa kisanii ambao hutegemea zaidi namna msanii alivyoziweka dhana hizo katika kazi yake.

Maelezo hayo ya Jilala yanatusaidia katika utafiti huu kuangalia dhana au maneno ambayo yamejitokeza zaidi kuliko mengine na pengine maneno hayo au dhana hizo ambazo zimejitokeza zaidi zinaweza kuwa ndizo zimebeba maana ya matini iliyokusudiwa na msanii. Pengine kwa maelezo hayo tunaweza kuona kuwa mchomozo unaweza kujitokeza katika takriri neno, takriri sentensi.

Wamitila (2008) anaeleza kuwa, mchomozo ni mbinu ya kudokeza mambo fulani katika kazi ya fasihi kwa namna ya wazi wazi na kufanya yajitokeze yakilinganishwa na mengine. Naye Van Peer (1980) anasema, mchomozo unaweza kueleweka kama dhana ya kipragmatiki inayorejelea uso-tuami wa mawasiliano kati ya mwandishi wa matini na msomaji. Pia Widdow (1975) anasema kuwa, mchomozo ni athari aipatayo msomaji itokanayo na isimu au namna nyingine za ukengeushi katika matini ya kifasihi.

### **2.4.1 Aina za Mchomozo**

Kwa kujumuisha mawazo yaliyotolewa na wataalamu hapo juu dhana ya mchomozo ni ujitokezaji wa vipengele vya kiisimu katika muktadha mahsusi wa kifasihi kwa wingi, uchache au kutotokeza kabisa kulingana na kaida au sharia zilivyo. Dhana ya mchomozo inaweza kujitokeza katika vipengele mbali mbali kama vile; takriri, usambamba pamoja na ukengeushi, ambapo takriri ni ujirudaji wa sauti, neno, sentensi, wazo au ridhimu fulani ili kuleta athari na maana maalum kwa msikilizaji au msomaji wa shairi au kazi ya fasihi wakati usambamba ni takriri ya sentensi au vifungu vya maneno vyenye kufanana kimaana au kimuundo vinavyojitokeza katika kazi za kifasihi.

Mbunda (1993:60), anaeleza kuwa, Takriri ni marudiorudio ya sauti, silabi neno, sentensi wazo au ridhimu; ili kulete athari kwa msomaji wa shairi linalohusika. Shairi hili lina aina za takriri zifuatazo: Takriri irabu, kononati, neno, mistari, muundo, vina, kituo, mizani/ silabi, rdhimu na mawazo. Naye, Wamitila (2010:486), amebainisha aina za takriri kuwa ni msamiati, irabu, konsonanti na vina. Vivyo basi, kwa mujibu wa utafiti huu tumetumia uainishaji wa Mbunda wa aina za takriri unaobaisha aina kumi (10). Lengo letu ni kupata zaidi kile ambacho msanii wa *Diwani ya Ustath Andanenga* amekifikisha kwa jamii yake.

#### **2.4.1.1 Mchomozo Takriri Irabu**

Wamitila (2010:486) anaeleza kuwa, urudaji unaopatikana hapa kimsingi ni urudaji wa kisauti. Takriri irabu hutokea pale ambapo sauti inayorudiwa au kukaririwa ni irabu. Naye, Mbunda (2010:61), anasema kuwa, ni marudiorudio ya irabu karibu kila

neni. Kwa mfano katika msitari wa kwanza pekee yake kuna takriri irabu za “a” au “e”

#### **2.4.1.2 Mchomozo Takriri Konsonanti**

Mbunda (2010:61), anasema kuwa, Marudiorudio ya Konsonanti pia yapo. Nayo yanafanana na marudiorudio ya irabu. Kwa mfano katika msitari wa kwanza kuna takriri konsonanti “l” au “p”...Takriri hizo za konsonanti zimeenea katika shairi zima.

#### **2.4.1.3 Mchomozo Takriri Neno**

Mbunda (2010:61) anaeleza kuwa, Takriri neno imetumiwa na mshairi kama mbinu ya kupamba na kuisitiza dhamira na maudhui yote kwa ujumla. Hivyo, takriri neno ni ujirudiajirudiaji wa neno ambao hujitokeza katika ubeti au ushahi mzima, ambapo neno moja hurudiwarudiwa.

#### **2.4.1.4 Mchomozo Takriri Mistari**

Mbunda (2010:61) anaeleza kuwa, Katika takriri hii kuna marudio ya mistari ile mine. Pili kuna takriri kituo, yaani marudio ya mistari wa kituo.

#### **2.4.1.5 Mchomozo Takriri Muundo**

Mbunda (2010: 61-62) Muundo wa shairi hili pia unarudiwa kutoka ubeti hadi ubeti.

#### **2.4.1.6 Mchomozo Takriri Vina**

Mbunda (2010: 62) anaeleza kuwa, Vina vinavyorudiwarudiwa katika shairi. Hivyo, silabi ambazo hujirudia katika ubeti huweza kujenga takriri vina.

#### **2.4.1.7 MchomozoTakriri Kituo**

Mbunda (2010: 62) anaeleza kuwa, mshairi amerudia kituo kilekile kutoka ubeti hadi ubeti. Hivyo, kile kituo kinachorudiwa kila ubeti huitwa Takriri Kituo.

#### **2.4.1.8 MchomozoTakriri Mzani/ Silabi**

Mbunda (2010:63) anaeleza kuwa,Shairi linapotumia mizani kumi na sita katika kila mstari. Kwa hali hiyo tunasema kuna takriri-mizani katika miastari hiyo.

#### **2.4.1.9 Mchomozo Takriri Ridhimu**


Mbunda (2010:63) anaeleza kuwa,Ridhimu ni mapigo katika shairi au wimbo. Hayo mapigo asilia kwa kawaida kila lugha ina mapigo yake. Ina mawimbi ya kupanda na kushuka na kwa kawaida mawimbi hayo huambatana na maana. Ushairi wa Kiswahili una ridhimu ambayo kwa asili yake inatokana na mazingira na shughuli za kibinadamu.

#### **2.4.1.10 MchomozoTakriri Mawazo**

Mbunda (2010:63)anaeleza kuwa, Mshairi anayerudia mawazo yaleyale kutoka ubeti hadi ubeti, ingawa pengine huleta wazo jipya.Takriri zote hizi hujenga taathira maalumu zinazoleta hisia Fulani.

#### **2.4.1.11 Dhima ya Mchomozo Takriri**

Mbunda (2010:64) Katika dhana ya mchomozo takriri, tunaweza kupata dhima mbalimbali, kwa mfano; husaidia kuonesha na kuelekeza mwenendo wa shairi, husaidia kupamba lugha, kusisitiza ujumbe na kufurahisha wasomaji.



**Kielelezo: Na 2.1: Uhusiano baina ya vipengele vya Mchomozo**

Chanzo: Mtafiti (2016)

#### 2.4.2 Mchomozo Ukengeushi/ Ukiushi

Jilala (2016:170) anaeleza kuwa, ukengeushi ni hali ya kutumia kaida tofauti ama kinyume na jinsi ilivyozoeleka katika utunzi ama uwasilishaji wa kazi za fasihi. Hii inamaana kwamba, ukiushi ni ukiukaji wa kanuni ama mazoea.

#### 2.5 Maudhui

Maudhui ni jumla ya mambo yote yanayowasilishwa katika kazi ya fasihi. Kipengele cha maudhui hujumuisha mambo kama vile dhamira, ujumbe, mtazamo, msimamo, falsafa na itikadi (Wamitila, 2008). Vilevile, Mbunda (1993:51) anaeleza kuwa, Ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, tenzi, mashairi...Kina ni mpangilio wa sauti za herufi. Amekubaliana na sifa za Ushairi zilizobainishwa na J.A. Ramadhani (2004) Mulika Na. 32 ambaye anazieleza sifa za msingi zinazohusu ushairi wa Kiswahili. Ramadhani anasema kwamba:

- i) Ushairi huanza na hisi au mchomo unaobainishwa na mazingira.
- ii) Hisi hizo huwasilishwa kwa msomaji kwa njia lugha teule ya kitamathali.
- iii) Hisi hizo lazima ziambatane na mawazo na mtazamo wa fikra.
- iv) Hali ya kishairi inahusiana kidogo na hali ya kindoto au tabia ya kuona yasiyoonekana na kuwania yasiyowezekana.
- v) Ushairi umefungamana na ubuni,na kwa hiyo hauwezi kuwekewa sharia zisizobadilika, na kwamba kuogopa kubuni kunadumaza maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.
- vi) Uwezo wa kubuni wa mshairi umetoka kwa Mungu ambaye ndiye mfalme wa Sanaa zote.
- vii) Shairi ni muungano wa fani na yaliyomo (maudhui).

Utafiti wetu tumelazimika kuoanisha sifa hizo za ushairi kwa vile kazi yetu vilevile ni kuchunguza Mchomozo unavyofikisha maudhui kwa jamii, mifano ni *Diwani ya Ustadh Andanenga*.

### **2.5.1 Ujumbe**

Christopher A.S(h.t) anasema, ujumbe ni jumla ya maono (impression) baada ya kusoma kazi ya fasihi. Kwa kawaida kila kazi ya fasihi huwa na ujumbe ambao msanii huwa amelenga kuufikisha kwa jamii aliyoilenga ambao ni wasomaji, watazamaji na wasikilizaji wa kazi hiyo ya kifasihi. Jilala (2016) anasema, ”ujumbe ni jumla ya maono baada ya kusoma kazi ya fasihi. Kwa kawaida kila kazi ya fasihi hubeba ujumbe ambao amelenga kuuwasilisha kwa jamii aliyoikusudia, yaani wasomoaji, wasikilizaji ama watazamaji wake. Katika kazi ya fasihi dhamira kuu

hubeba ujumbe wa msingi na dhamira ndogo ndogo hubeba ujumbe ambao husaidia kuujenga au kuupa uzito ujumbe wa msinigi”.

Mbunda (1993:58), anaeleza kuwa, Maudhui ni jumla ya mambo yanayoelezwa ama kujitokeza katika kazi ya kifasihi. Maudhui ya kazi ya fasihi hujumuisha dhamira, mtazamo ama msimamo, ujumbe, maadali na falsafa.

Mwandishi yeyote wa kazi ya fasihi huwa na jambo ambalo amekusudia alifikishe katika jamii yake, pengine akiitaka jamii yake iweze kubadilika. Hivyo, hutoa mafundisho kwa njia mbalimbali akiwa na lengo la kuielimisha jamii yake ifikie yale aliyoyakusudia.

## **2.6 Pengo la Maarifa**

Pamoja na kuwa kuna tafiti ambazo zimefanywa kuhusu ulinganishaji wa kazi za Ushairi, lakini ulinganishaji huo japo ulizingatia masula ya Fani, lakini si kazi moja ya mwandishi mmoja. Vilevile, tafiti nyingi zimejikita katika kulinganisha fani na maudhui ya kazi za fasihi. Hivyo, bado kuna umuhimu wa kufanya utafiti juu ya vipengele vya Mchomozo, kulinganisha na kulinganua, katika kazi ya mwandishi mmoja. Pengo hili ndilo ambalo limekusudiwa kuzibwa katika utafiti huu. Ili kufikia lengo hilo, utafiti huu basi, utajaribu kuziba pengo hilo kwa kuchunguza vipengele vya Mchomozo katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*.

## **2.7 Dhana ya Nadharia**

Wafula & Kimani (2007:2), wanasema kuwa, Nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi kuifahamu

kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Nadharia ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani. Hii ina maana kuwa , Nadharia inaweza kutokana na mawazo yaliyoundwa kitambo na jopo la wataalamu au inaweza kutokana na usomaji makini wa kazi fasihi na mtu binafsi.

Wamitila (2010:1) anaeleza kuwa, Nadharia ni maarifa ya kitaaluama ambayo msomaji au mhakiki anapaswa kuyajua na kuyafahamu kabla ya kuanza kazi yake. Haya ni maarifa ambayo inatupasa kuwa nayo kabla ya kujihusisha na kazi ya uhakiki. Ni maarifa ambayo yatamwezesha msomaji pia kuyaelewa mambo muhimu, na kwa nja hiyo kuuboresha usomaji wake na uwezo wake wa kufurahia fasihi. Tunakubaliana na maelezo ya Wafula & Kimai (2007:2) kuwa nadharia ni mwongozo unaomwezesha msomaji wa kazi ya fasihi kuifahamu kazi ya fasihi na vipengele vyake vyote. Na katika kazi yetu hii tumechukulia nadharia kuwa ni mwongozo unaomwongoza msomaji wa kazi ya fasihi kuweza kubainisha vipengele vya fani na maudhui.

## **2.8 Kiunzi cha Nadharia**

Katika utafiti na uchunguzi wa kazi za fasihi, zipo nadharia mbalimbali ambazo zinaweza kutumika kuchunguza na kuchambua kazi za fasihi. Aidha, ni dhahiri kuwa, kila nadharia inaweza kufaa ama kutofaa kuzichambua kazi za fasihi kwa kuzingatia lengo la utafiti. Katika utafiti huu tungeweza kutumia nadharia za fasihi kama vile nadharia ya Elimu mtindo, *sosholojia*, *saikolojia changanuzi*, *mwitikio wa msomaji*, *umaksi* na *korasi* hizi zikiwa ni baadhi tu ya nadharia.



Hata hivyo, nadharia hizi zilionekana kutofaa katika kuchunguza na kuchambua data za utafiti huu kutokana na malengo ya utafiti huu. Hivyo basi, kulingana na malengo ya utafiti huu, “*Nadharia ya Umaksi (Marxist theory)*” imeonekana kuwa inaweza kufaa na kutuongoza katika kuchunguza na kuchambua data za utafiti huu. Nadharia ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani (Mdee na wenzake) kwa mawazo hayo nadharia hubeba mawzo, dhana au maelezo yanayotolewa kwa nia au kwa lengo la kueleza hali fulani, chanzo, muundo utendaji na mwingiliano wa jambo fulani kwa kawaida na kwa kina zaidi. Sengo (2009) anafasili nadharia kuwa ni mwongozo mkuu wa mtu, watu au jamii ya pahala fulani. Kwa maana hiyo nadharia ni sawa na itikadi ambayo huwaongoza jamii fulani kiuchumi, kisiasa, kidini na kiutamaduni ili kuendesha jamii husika. TUKI (2004) Nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kuelekeza jambo fulani. Tunanakubaliana na maana iliyotolewa na Tuki, kutokana na fasili yao imetaja mambo muhimu kama vile maelekezo, mawazo na mwongozo ambao utamwongoza na kumsaidia mhakiki ili kutatua tatizo fulani.

## **2.9 Nadharia ya Umaksi ( Marxist theory)**

Nadharia ya Umaksi ilianzishwa na Karl Marx mwaka (1818-1863) na Fredrich Engles (1820-1895). Katika nadharia hii Marx amejikita zaidi katika historia na miundo ya kijamii kwa kupitia hoja mbali mbali. Kwanza, historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi ya kiyakinifu ya kiuchumi ambayo itachunguza njia za uzalishaji mali na usambazaji wa mali hizo. Hivyo vyote huunda msingi unaojiegemeza katika maadili, itikadi, dini na utamaduni. Pili, historia ya

maisha ya binadamu yanaakisi harakati za kitabaka za kiuchumi-jamii. Marx anasema; 'Historia ya maisha ya binadamu niya harakati za kitabaka.' Harakati za kitabaka katika jamii. Chombo (2014). Nadharia ya Ki-marx inaangalia matabaka katika ngazi mbali mbali za kijamii kama vile, ngazi ya familia, dini, elimu na kitaifa. Na hivyo kwa mujibu wa Marx ni jukumu la tabaka tawaliwa kujikwamua ili kuondokana na kugandamizwa na tawala.

Kimsingi, mabadiliko ya mfumo wa kiuchumi wa kijamii ndiyo msingi wa mabadiliko ya mfumo wa maisha katika jamii na muundo wa utawala. Kwa mfano, kuanzishwa kwa soko huria kilikochangiwa na utandawazi kumebadili mfumo ya maisha ya jamii na kuleta utabaka wa hali ya juu.

Wamitila (2002:183), anaeleza kuwa, wahakiki wa Ki- Marx wanaamini kuwa daima historia ya binadamu inadhahirisha na kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi –jamii. Itakumbukwa kuwa Karl Marx alisema kuwa historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka... Kitu cha msingi katika maisha ya binadamu ni kula na kunywa, kupata malazi na mambo mengine.

Kutokana na harakati hizo binadamu hupambana ili aweze kujikomboa na apate unafuu wa kimaisha kuliko alipokuwa mwanzo. Nadharia ya Ki-marx inaangalia na kuichunguza historia ya jamii katika mtazamo wa hali halisi na kuiona jamii ikiwa katika mfumo wa kitabaka, ambao huathili hata uzalishaji mali katika jamii husika. Hivyo basi katika fasihi na ikiwa fasihi ni zao halisi la jamii husika na fasihi huaksi hali halisi iliyomo katika jamii. Basi, hata mwandishi katika kuandika kazi yake

ataisawiri jamii katika kuaksi hali halisi ya kitabaka iliyomo katika jamii husika. Vile fasihi inaweza, pia kuonesha matatizo yaliyomo katika jamii husika kwa vile fasihi huaksi uhalisia wote utendwao na jamii husika.

### **2.9.1 Sifa Za Uhakiki wa Kimarx**

Kuwa na mwelekeo wa kuitazama sanaa kwa kutumia nadharia hii kwa kutilia mkazo dhamira. Tunatilia mkazo dhamira kwa sababu ya matamano yaliyomo katika jamii. (matamano ya wanyonge na matajiri ni yapi?).

- Ni mkabala unaoiangalia fasihi kwa kuishusisha na mazingira yake ya kihistoria pamoja na shughuli zingine za kibinadamu.
- Ni nadharia inayopinga mtazamo wa kubagua au kutenga fasihi na mazingira yanayoizaa, kama ilivyoonyeshwa katika nadharia zingine kadhaa. Chombo (2014)

Kwa kuhimiza kuchunguzwa kwa vipengele vya kijamii na uchumi, uhakiki umepanua uwanda wa fasihi.

Wafuasi wa *nadharia ya Umaksi* wanaamini pia kwamba unapotumia Nadharia ya Ki-marx katika uhakiki wa kazi za kifasihi, lengo kubwa ni kuonesha tofauti za kiuchumi, kisiasa, kijamii kulingana na maelezo yalivyo katika kitabu. Hivyo basi kazi hii itachunguza tofauti za kiuchumi, kisiasa na kijamii zilivyoweza kujitokeza na kuibua maudhui ya kufanana au kutofautiana kwa mtunzi wa *Diwani ya Ustadh Andanenga*.

### **2.10 Hitimisho**

Sura hii imejadili kuhusiana na kazi tangulizi ambayo imeonesha namna ambavyo

watafiti wengine walivyofanya utafiti kuhusiana na mambo kadhaa ya kifasihi, ambapo mtafiti alichagua kazi za kiutafiti ambazo zinamwelekeo na kazi ya kiutafiti anayoifanya ili kufahamu nini walifanya, wakagundua nini, wakachambua je, na tatizo lilikuwa ni nini, pengo la maarifa na hatimaye maarifa gani mapya waliyoyaweka wazi kutumika katika taaluma ya fasihi. Katika sura hii ilianza na kazi tangulizi katika kuchunguza dhana ya *fasihi linganishi* ambapo wataalamu kama vile wallek (1988), Bassnett (1993) na Guyard kama alivyonukuliwa na Weisstein (1968) walijadiliwa mawazo yao na kuonekana kipi ambacho hakijafanyika ambacho utafiti huu utakiibua.

Pia katika sura hii mtafiti ametalii kazi tangulizi zinazozungumzia suala la mchomozona maudhi kwani utafiti wetu unazungumzia vipengele vya mchomozo. Utafiti huu umetumia *nadharia ya Umaksi*, katika uchambuzi wa matini itazungumzia kuhusu kufaa kwake katika kuchunguza vipengele vya mchomozo vinavyofiksha maudhui kwa jamii husika. Sura inayofuata ni sura ya tatu. Sura hii inahusu mbinu za utafiti.

## **SURA YA TATU**

### **3.0 MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii inajadili mkabala wa utafiti, mbinu, na vifaa ambavyo vilitumika katika utafiti huu. Utafiti huu umetumia mkabala wa kitakwimu na usio wa kitakwimu katika kukusanya na kuzichambua data za utafiti huu. Kama wanavyoeleza (Kombo na Tromp, 2006) kuwa, utafiti wa kitakwimu na usio wa kitakwimu hujazilizana na kukamilishana. Kwa maana hiyo, utafiti huu utahusisha maelezo ya data na pia utatumia nduni za utafiti wa kitakwimu. Hivyo, sura hii inajadili kuhusu mbinu za utafiti na hatua zitakazotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu.

#### **3.2 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu umefanyika katika eneo la jiji la Dar es Salaam, ambapo maeneo kadhaa yalichaguliwa na kutumika kulingana na mahitaji ya utafiti huu. Maeneo hayo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania jijini Dar es Salaam. Tumeteua maeneo hayo kwasababu ya urahisi wa upatikanaji wa maktaba za kutosha ambapo upatikanaji wa vitabu vilivyotajirisha utafiti huu ulikuwa rahisi. Katika maeneo hayo tumepata Maktaba kuu ya Tanzania, maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, Dar es Salaam ni eneo ambapo wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili hupatikana hususani tamthiliya ya Kiswahili ambapo kwa kupitia mawazo yao utafiti huu ulifikia malengo yake. Dar es Salaam ni eneo ambalo mtunzi wa kazi za fasihi

tutakayoitumia katika utafiti huu hupatikana. Katika eneo hili la Kinondoni Manyanya msanii *Amir A. Sudi Andanenga* hupatikana maana ndiyo makazi yake.

### **3.3 Mbinu ya Usomaji wa Maktabani**

Mbinu ya usomaji wa maktabani huhusisha kutafuta data kwa kusoma vitabu mbalimbali kama vile vitabu teule, tahakiki, majarida, na vitabu vya ziada kulingana na malengo ya utafiti ili kupata data zitakazo kidhi haja ya kiutafiti. Mbinu hii imetumika katika utafiti huu ambapo mtafiti alisoma na kuchambua vya *Diwani ya Ustadh Amir A. Sudi Andanenga*, pamoja na vitabu vingine vya ziada ambavyo vimewezesha kupata taarifa za muhimu katika utafiti huu. Kwa kusoma vitabu hivyo vilivyopatikana katika maktaba na maduka ya kuuza vitabu mtafiti ameweka bayana vipengele vya kimchomozo katika *diwani ya Ustadh Andanenga* na hivyo ameweza kubainisha maudhui yanayobainishwa na msanii kupitia vipengele vya mchomozo. Mbinu hii ni bora kwani maktabani unaweza kupata vitabu na majarida yanayozungumzia kile unachotafiti na pia kupata mawazo ya ziada kuhusiana na wengine walivyoshughulikia tatizo hilo. Mbinu hii imefaa sana katika utafiti huu na iliweza kujitoshaleza.

#### **3.3.1 Matini**

Kipo kitabu ambacho kilitumika katika utafiti huu kwa ajili ya kuchunguza na kubainisha vipengele vya mchomozo na maudhui yanajitokeza katika *Diwani ya Ustadh Andanenga* na vitabu vingine kama vya kihakiki ambapo matini hizi zimetusaidia kupata mchango mkubwa katika utafiti huu, kwani data za kimaudhui zimepatikana na kufanikisha utafiti huu.

### 3.2.2 Uchambuzi wa Data

Data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mbinu mbili, ambazo ni *uchambuzi linganishi* na *uchambuzi maudhui*, japo tunafahamu kuwa zipo mbinu nyingine ambazo zinaweza kutumika katika kuchambua data za utafiti wa namna hii. Pia tukiweka bayana kuwa utafiti huu una sifa za utafiti usio wa kitakwimu na utafiti wakitakwimu. Katika uchambuzi, mtaalamu Tromp (2006) anaelezea kuwa uchambuzi maudhui ni mbinu ya uchambuzi ambayo huziweka mada kulingana na jinsi zinavyofanana na kuhusiana ambapo dhamira zilizobainishwa huwekwa pamoja kukidhi haja ya kiutafsiri wa data. Katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu hii kwani inamfaa katika kufikia malengo yake ambapo uchambuzi vipengele vya mchomozo umemsaidia kupata maudhui katika kazi ya kiusanii na kuona namna gani vipengele vya mchomozo vinavyotumika katika kuweka bayana maudhui yaliyojitokeza. Uchambuzi linganishi ni mbinu ambayo mtafiti ameitumia katika utafiti huu katika kulinganisha data kutoka katika vyanzo mbalimbali kama maktaba na matini ili kupata majumuisho ya namna ambavyo vipengele vya kimchomozo vilivyotumiwa na msanii huyo. Katika utafiti huu mtafiti alifanya yafuatayo katika uchambuzi wa data:

- Kuchambua vipengele vya mchomozo katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*.
- Kuchambua jinsi ambavyo vipengele vya mchomozo vinavyofikisha maudhui katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*.

### 3.3 Hitimisho

Sura hii imejadili juu ya mbinu za utafiti, ambapo eneo la utafiti limebainishwana uchambuzi wa data. Katika ukusanyaji wa data mbinu ya usomaji wa maktaba

imetumika kiufanisi. Katika uchambuzi wa data kwa kutumia mbinu mbili ambazo ni uchambuzi maudhui na uchambuzi linganishi. Sura inayofuata ni sura ya nne. Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data.



## SURA YA NNE

### 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

#### 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizokusanywa katika utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza inahusu vipengele vya mchomozo katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*, sehemu ya pili inajadili juu ya dhima ya vipengele vya mchomozo katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*. Sehemu ya tatu inajadili ulinganuaji wa vipengele vya Mchomozo na Sehemu ya mwisho ni hitimisho.

Katika msingi wa nadharia ya Ki-Marx, uhalisia huu ni mivutano ya kitabaka na mifumo ya uzalishaji mali pamoja na mahusiano ya kipembuzi ya kati ya jamii yenyewe na historia ya jamii yetu. Hivyo uchambuzi wetu utazingatia vipengele vya mchomozo nauhalisia huu wa mivutano ya kitabaka uliopo katika jamii ya Kitanzania kupitia *Diwani ya Ustadh Andanenga*. Lengo ni kuona vipengele vya mchomozo vilivyotumika kuwasilisha maudhui yapi kwa jamii husika.

Hivyo kwa mujibu wa utafiti huu tutachambua vipengele vitatu vya mchomozo ambavyo ni ; takriri, usambamba na ukengeushi.

#### 4.2 Uteuzi na Matumizi ya Vipengele vya Mchomozo

Katika utafiti huu, vipengele vya mchomozo ambavyo vimebainishwa katika utafiti huu ni pamoja na takriri na aina zake, usambamba na aina zake, na ukengeushi.

Kama lilivyo lengo letu la kwanza katika utafiti wetu ni kubainisha vipengele vya mchomozo katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*, ufuatao ni ubainishaji huo kwa diwani hiyo.

#### **4.2.1 Mchomozo katika Diwani ya Ustadh Andanenga**

Katika kubainisha vipengele vya mchomozo katika Diwani ya Ustadh Andanenga, tumeanza na kipengele cha takriri na aina zake ambazo ni; takriri neno, silabi/sauti, na sentensi.

##### **4.2.1.1 Mchomozo Takriri katika Diwani ya Ustadh Andanenga**

Ni mchomozo unaojitokeza kama neno, sauti, au sentensi ambayo hujirudia rudia kama msisitizo wa jambo. Katika Diwani ya Ustadh Andanenga mbinu hii imejitokeza kama ifuatavyo:

###### **4.2.1.1.1 Mchomozo Takriri Neno**

Kama tulivyokwisha kueleza kuwa, Takriri neno ni urudiaji wa neno moja katika ubeti, shairi au katika mshororo. Utafiti huu umeweza kubainisha mifano ya Takriri neno ifuatayo:

Mifano ya mchomozo takriri neno ambayo utafiti huu umebaini katika shairi la “Mvunja kwao ni Jura” ni :

*Nakana hana thamani, mvunja kwao ni jura  
Tene jura hadharani, na kila anakogura  
Mvunja kwao ni jura, muradi hana thamani.*

Maneno kama’ hana, thamani, mvunja, kwao na jura’ yamejitokeza kama mchomozo takriri neno katika shairi la Mvunja kwao.

*Leo makusudi yangu, nataka kusimulia  
Kusimulia wenzangu, wote mnaosikia  
Na ingawa wengi tangu, kura wanafurahia  
Tusipuuzze raia, haki ya kupiga kura  
Ni kwa furaha pasipo, nyumanyuma kujikita*

Katika shairi la ‘Haki ya kupiga kura’ maneno kama ‘kusimulia’, ‘kura’, na ‘wanafurahia’ yamejitokeza kama mchomozo takriri neno.

*Walisema takataka, mila zenu mila gani  
Na hadithi vilevile, ziwemo humu kundini*

Katika shairi la ‘Tusifu Utamaduni’ maneno kama ‘takataka’ ‘vilevile’ na ‘mila’ yamejitokeza kama mchomozo takriri neno. Yametumika hivyo ili kulete msisitizo katika kusesitiza wanajamii tusamini utamaduni wa Kitanzania.

*Bismilahi kuchora, kuchora ni kuandika  
Kuandika ya busara, ndiyo hasa ninataka  
Ili yapate someka  
Someka nilotongora, kadri yatakofika  
Taifa bila shamra, katu halitaongoka  
Taifa litajengeka, kwa bidii za wakazi.  
Ninasema ya hakika  
Hakika ya viongozi, yao wanayo tamka.  
Tujitowe kila mtu, tujitowe si dhihaka  
Ili tupate fanaka  
Fanaka ya nchi yetu, hakuna kama kufyeka  
Kufyeka yetu misitu, tupande nyingi nafaka  
Hatuzami chini aka  
Aka hatutasomewa, nawaapia Rabuka  
Lakini sina mashaka  
Mashaka yatatuchoma, na mazito kujitwika  
Bila ya kupumzika  
Kupumzika huachwa, bali wanahangaika*

Katika shairi la ‘Ujengaji wa Taifa’ maneno kama vile; ‘kuchora’, ‘kuandika’, ‘someka’, ‘taifa’, ‘hakika’, ‘tujitowe’, ‘fanaka’, ‘kufyeka’, ‘aka’, ‘mashaka’, na ‘kupumzika’ yametumika kama mchomozo takriri.

*Jaribu tukijaribu, kweli tutafanikiwa  
Mwisho tutafanikiwa, ikiwa tutajaribu.*

Katika shairi la ‘Jaribu Tukijaribu’ maneno kama vile ‘tukijaribu’ na ‘tutafanikiwa’ yametumika kama mchomozo takrir neno.

*Uchumi tunaposema, neno hili kila mara  
Maana yake huduma, ziletazo itijara  
Katika nchi nzima, toka pwani hadi bara  
Uchumi ni biashara, viwanda na ukulima  
Biashara zilo njema, siyo kwenye barabara*

*Na kilimo hima-hima, eka nyingi siyo dhira  
Haya yatakapo shikamana, nasi tutatia fora  
Fora mpaka kiyama, mengine tutasomewa.*

Katika shairi la ‘Uchumi’ maneno kama vile; ‘uchumi’, ‘biashara’, ‘hima-hima’ na ‘fora’ yametumika kama mchomozo takriri neno.

*Nchi zilizofaulu, mambo mengi kemukemu*

Katika shairi la ‘Awazalo Binadamu’ neno ‘kemukemu’ limejitokeza kama mchomozo takriri neno.

*Swali kubwa ililopo, kujitegemea nini?  
Na taifa huwa duni, bila kujitegemea*

Katika shairi la ‘Kujitegemea’ neno ‘Kujitegemea’ limejitokeza kama mchomozo takriri neno.

*Mwenge katika vijiji, vya ujamaa pitia  
Mwenge mulika mitaji, umma kutufaidia  
Mwenge ruka kwenye maji, Unguja kuzunguka*

Katika shairi la ‘Mwenge’ neno ‘Mwenge’ limejitokeza katika beti zote kama mchomozo takriri neno.

*Katika nchi za watu weusi, tuzijenge zijengeke  
Tuzijenge zijengeke, nchi za watu weusi.  
Kila jema tuabesi, baya tulipige teke  
Teke la nguvu kwa kasi, tupigalo lipinduke*

*Nchi za watu weusi, majungu tusiyapike  
Majungu ya wasiwasi, kama jahazi tutweke'*

Katika shairi la 'Nchi za watu weusi' maneno kama ' watu weusi', 'tuzijenge', 'zijengeke', 'teke', 'wasiwasi' na ' majungu' yamejitokeza kama mchomozo takriri neno katika kuweka msisitizo wa kufikisha ujumbe wa ujenzi wan chi za kiafrika kwa kujituma katika kazi.

*Tuondoe petupetu, pamoja na zile dhiki.  
Tuwemo ushirikani, tuinge unyonyaji  
Kwa kupinga unyonyaji, tuwemo ushirikani  
Na tuchange moja moja, si lazima hamsini  
Ushirika kitu chema, aidha kina thamani  
Thamani kwa sisi umma, na uchumi kwa nchini.*

Katika shairi la 'Ushirika' maneno kama 'petupetu', 'unyonyaji', 'ushirikani', na 'thamani' yamejitokeza kama mchomozo takriri neno.

*Hiyo naapa Baratu, yafaa kurekebisha  
Turekebishe wabantu, na njia njema kunyosha  
Kwamba tulime misitu, na mimea kuotesha  
Mikonge na kila kitu, tupande na kuotesha.*

Katika shairi la 'Dhamira ya nchi yetu' maneno kama vile; 'Baratu', 'kurekebisha' na ' kuotesha' yametumika kama mchomozo takriri neno.

*Tenda si kusimulia, wasifu wa Ujamaa.  
Wakapingwa palepale, leo wanazingatia  
Ujamaa uwe tengu, nyapara wawe sawia  
Kazaliwa mkombozi, wa kondoo wapotevu  
Wa kondoo wapotevu, kazaliwa mkombozi  
Yesu alijizalia, kwa kazi ya Ukombozi  
Kazaliwa mkombozi, wa kondoo wapotevu.  
Nimefika kaditama, mwisho wa masimulizi  
Nawapisha mahashama, watowe masimulizi.  
Serikali twabembeleza, Tafadhali tafadhali  
Hivyo lugha Kiswahili, ni la mama ziwa kama  
Kama tukinyonya hili, na mengine tukakoma  
Itasitawi miili, na kuponywa homahoma*

*Uzuri wa lugha yetu, kutopindama pindama.  
Heko bingwa wa kitali, sasa umetengeneza  
Heko isiyo mithili, wema mwingi umeijaza*

Maneno kama vile, ‘mkombozi’, ‘mkombozi’, ‘wapotevu’, ‘kazaliwa’, ‘kondoo’, ‘kaditama’, ‘tafadhali’, ‘mama’, ‘homahoma’, ‘pindama’ na ‘heko’ katika shairi la ‘Kazaliwa Mkombozi’ ‘Heko Kawawa Mkuza’ na ‘Kiswahili mama’ yamejitokeza kama mchomozo takriri neno.

*Tukitaka tuongoke, lugha tusiombe-ombe  
Lazima tukusanyike, kila pembe hadi pembe  
Ili tusiaibike, haya harambe harambe*

Maneno kama ‘tusiombe’, ‘pembe’ na ‘harambe’ yametumika katika shairi la ‘Kiswahili Tukipambe’ kama mchomozo takriri neno.

*Bidii mbaya zikombwe, zibakie nyonde nyonde  
Zicheze kindumbwe ndumbwe, na ziunguwe matende.  
Kuuhani ushairi, washairi yatubidi  
Washairi yatubidi, kuuhani ushairi  
Mkongo hima walani, walazwe kifudifudi  
Washikwe hawa washikwe, wacharazwe mijeledi  
Hawa watu majahili, rangi zao pelepele  
Tupo wawili wawili, kwa kupiga vita vile.  
Hutafika kwenye goli, utazama polepole  
Nasema sipendelei, kwa tungo mmekithiri  
Kuyele na Bushiri, tungo zenu zaridhisha  
Niliwambieni tunga, humu humu Ngurumoni  
Kwamba pindungupindungu, ja ngalawa baharini  
Walaji waje wenyewe, waje kula hadharani  
Mkuu kwa mapotozo, moyo hapa duniani  
Kila baa duniani, moyo ndiye muongozo  
Kama ndo yale maoni, UKUTA mliopeana  
Ukuta uzomwa kwani, unipe jibu kijana  
Hadi tufikie kengo, kengo yenye ubaridi  
Hasa langu kusudio, ni ukweli siyo soga  
Ukweli ni kamatio, ja- mikono na mabega  
Shuku huvunja ujima, shuku ni jambo la mkosi  
Shuku kibaya kilema, kitiacho wasiwasi  
Vuta kamba hima hima, tupe unavyo yahisi  
Awe baba awe mamba, kwa kuwa yeye mtesi*

*Uso ukimtazama utamwona posiposi  
 Mbumbumbu bali anasa, gari zinatuchukia  
 Maneno yenye kipyangu, kunena kwangu jitenge  
 Kunena jitenge kwangu, mfano wa lile genge  
 Hadhiyo ya Sungusungu, mla chembe siyo tonge  
 Utunzi wa bangu bangu, kuwa nyumba ya mshonge  
 Wa kafukafuja kungu, tungile zongemazonge  
 Kichongo kingindo dungu, zongemazonge*

Katika kifungu cha maneno hayo , kuna maneno kadhaa ambayo yametumiwa kama mchomozo takriri neno,. Mfano wake ni; ‘pindungupindungu’, ‘ waje’, ‘moyo’, ‘ moyo’, ‘ duniani’, ‘ukuta’, ‘kwangu’ ‘kunena’ ‘kengo’, ‘ukweli’, ‘shuku’, ‘hima hima’, ‘ awe’, ‘posiposi’, ‘mbumbumbu’, ‘jitenge’, ‘ sungusungu’ ‘zongemazonge’ na ‘ bangu bangu’.

*Mtu mtu kweli Yule, mjua lile na hili  
 Mjua lile na hili, mjaza tele  
 Tele akili timamu, lile hili mjulie  
 Na dunia ni mwalimu, mama baba vilevile  
 Mgeni kumi kwa kumi, makisi uzipatile*

Katika shairi la ‘Jitenge’ maneno kama ‘mtu’, ‘mjua’, ‘lile’, ‘hili’, ‘tele’, ‘ vilevile’ na ‘kumi’ yamejitokeza kama mchomozo.

*Jinga ni jinga la moto, lifukalo liwakalo  
 Msitu huu mnene, nausifia Amiri  
 Umejeza pande nne, kwa miti yake mizuri imenewiri  
 Imenawiri ione, imejeza mema furi  
 Tusiende ovyo ovyo, bila ya kuwa mahiri  
 Mbele tutatahari  
 Tahayari ni juavyo, si neno la kutabiri  
 Atafanya bilikuli, ndege apate kuhama  
 Tundu bovu afadhali, la zama zile za zama  
 Nyenza ziwe mbalimbali, si imara kwa kufuma  
 Yarabi ndiye Jalia, Yarabi Yarabi Mungu  
 Hamtaki kufyagia, kuondoa chunguchungu  
 Wa Madhehebu ya punda, yafaa kumkiuka  
 Wa Madhehebu ya chui, jitenge nae  
 Yafaa kumkiuka, kwani huyo ni adui  
 Ni kweli sio dhihaka, atakuua ja ndui*

*Panzi wanapopigana, kunguru wa kufurahani  
 Kunguru hunona sana, tena hutia ubani  
 Vita vizidi upana, maiti ziwe chunguni  
 Kunguru wapo vitani, vindindi bahati yao  
 Aheri ya wote nyoka, kulikoni nyoka mbito  
 Kulikoni huyu mbito, akheri ya wote nyoka  
 Tamati ya mot omoto, hapa chini ninaweka  
 Umbea kusema babu, umbea magaragaza  
 Leo tena nahitaji, nataraji Andanenga  
 Kutimiza mahitaji, yaruke katika anga  
 Kama ni maneno bora, haya niliyoyatunga  
 Maradhi bora kukinga, usingojee kponya.  
 Kujuwana tujuwana, tujuwane inabidi  
 Inabidi tupendene, tupendene makusudi*

Katika kifungu cha maneno hapo juu, maneno kama, 'jinga', 'moto', 'tutahayari', 'madhehebu', 'Yarabi', 'kunguru', 'vita', 'aheri', 'nyoka', 'motomoto', 'chungu', 'umbea', 'nahitaji', 'bora', 'kujuana', na 'tupendane' yametumika kama mchomozo takriri neno kuweka msisitizo na kufikisha ujumbe wa matini, ambao ni pamoja kujenga undugu miongoni mwa raia wan chi husika.

*Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu  
 Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja  
 Ulimwengu ni kiwanja, cha wenye tabu na raha  
 Bali ni moyo wa mtu, alojali Jalaa  
 Asiye moyo wa kutu, hutoa yake adaa  
 Si utajiri kata, katika kutowa kitu  
 Katika kutowa kitu, si utajiri kata  
 Umeuliza ni nani, mkuu wa mapotozo  
 Mkuu wa mapotozo, moyo hapa duniani  
 Moyo hutia motoni, akhera kwa mazungumzo  
 Wema ni kitu buruji, popote ni muangazo  
 Kwani wema ndiyo chanzo mtu kuijua miji  
 Mungu atupe uwezo, mimi na mtangazaji  
 Makarani mahafuzo, Mungu kawapiga geji  
 Wema kwa Mola agizo, soma katika miraji  
 Hilo lake Mola pazo, kwenu kama ni fariji  
 Kuzingatia ni sifa, ni sifa ya kiwalii  
 Ushairi ni maghani, za Washairi riwaya  
 Riwaya ziko moyoni, zikaja athiri taya  
 Dini ajali kifaya, faradhi zake Rabia  
 Faradhi zake Rabia, dini ajali kifaya*



*Wema mtendee ng'ombe, mpe majani mazuri*  
*Mbwa kumbuka wema, hakika yu mjasiri*  
*Mapenzi ya shombo, sitavumilia*  
*Mapenzi ni ladha, iso mithirika*  
*Lumbata mmoja, pendo la mashaka*  
*Pendo makuri, halina shikio*  
*Pendo la pesa si pendo, mbali nalo jitenge*  
*Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.*  
*Kimada kakosa haki, kwani si ndoa kamili*  
*Halingani na wa ndoa kimada kakosa haki*  
*Ulo bora mno, kasha imara*  
*Ulo na maono, kuwa ni dira*  
*Likampate Robati, fukizo la manukato*  
*Fukizo la manukato, likampate Shabani*  
*Urefu wa potopoto, si mwema tisa tamati*  
*Hakika kifo kikubwa, kafa Kluta Abedi*  
*Kwa kufa Sheikh Abedi, mlezi wa lugha yetu*  
*Kimefiwa Kiswahili, kufa Bwana Mathias*  
*Kufa Bwana Mathias, kimefiwa Kiswahili*  
*Ai! Msiba muone, wa kututoa kamasi*  
*Ai! Jamani jamani, tumeondokewa sisi*  
*Molina tupe nguvuzo, na nguvunimo fahamu*  
*Na fahamu tupazo, ziwezo zenye elimu*  
*Molina tupe nguvuzo, na nguvunimo nujumu*

Maneno kama ; ‘ Ulimwengu’, ‘ kiwanja’, ‘ moyo’, ‘ utajiri’, ‘ kata’, ‘ kutoa’, ‘ kitu’, ‘ mkuu’, ‘ mapotozo’, ‘ penndo’, ‘ akhera’, ‘ wema’, ‘ Mungu’, ‘ Mola’, ‘ riwaya’, ‘ Rabia’, ‘ mapenzi’, ‘ pendo’, ‘ pesa’, ‘ kimada’, ‘ ndoa’, ‘ ulo’, ‘ Molina’, ‘ manukato’, ‘ potopoto’, ‘ kafa’, ‘ Abedi’, ‘ kufa’, ‘ Mathias’, ‘ Kiswahili’, ‘ fukizo’, ‘ ai!’, ‘ jamani’, ‘ fahamu’ na ‘ Molina’.

#### **4.2.1.2 Takriri Mistari**

Mbunda (2010) anaeleza kuwa, Katika takriri hii kuna marudio ya mistari ile minne.

Pili kuna takriri kituo, yaani marudio ya mstari wa kituo. Katika diwani ya *Ustadh Andanenga*, mchomozo wa takriri mistari umejitokeza katika mashairi mbalimbali.

Mfano wake ni huu ufuatao:

Katika shairi la ‘Mvunja kwao’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Mvunja kwao ni jura, muradi hana thamani’.

Katika shairi la ‘Haki ya kupiga kura’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Tusipuuze raia , haki ya kupiga kura’.

Katika shairi la ‘Azimio la Arusha’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘ Safari tumeazimu, kwenda kwenye Ujamaa’.

Katika shairi la ‘Tusifu Utamaduni’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘ Tusifu utamaduni, wetu wa Kiafrika.

Katika shairi la ‘ Ujengeji wa Taifa’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Taifa litajengeka kwa bidii za wakazi.

Katika shairi la ‘Jribu tukijaribu’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘ Jaribu tukijaribu, kweli tutafanikiwa.

Katika shairi la ‘Uchumi’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Uchumi ni biashara, viwanda na ukulima’.

Katika shairi la ‘Awezalo Binadamu’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘ Awezalo binadamu, tusingeme hatuwezi’.

Katika shairi la ‘Katika kujenga nchi’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Katika kujenga nchi, tusingoje kutendewa’.

Katika shairi la ‘Kujitegemea’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Na taifa huwa duni, bila kujitegemea’.

Katika shairi la ‘Mapinduzi’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Maana ya Mapinduzi, kutafuta hali njema’.

Katika shairi la ‘Mwenge’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Angaza Tanzania, kote unakaribishwa’.

Katika shairi la ‘Nchi za watu weusi’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Tuzijenge zijengeke, nchi za watu weusi’.

Katika shairi la ‘Tuiunde nchi yetu’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Shime tuondoe chuki, tuiunde nchi yetu’.

Katika shairi la ‘Ushirika’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Tuwemo ushirikani , tuupinge unyonyaji’.

Katika shairi la ‘Dhamira ya nchi yetu’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Kuweka mbele maisha, dhamiri ya nchi yetu’.

Katika shairi la ‘Ujamaa’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Tenda si kusimulia, wasifu wa Ujamaa’.

Katika shairi la ‘Viapo’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Walaniwe na Karima, wapendao kula viapo’.

Katika shairi la ‘Kazaliwa Mkombozi’ mchomozo takririni ‘ Kazaliwa mkombozi ,wa kondoo wapotevu’.

Katika shairi la ‘Kitangazwe Kiswahili’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Juu kiwe Kiswahili, chini kiwe Kiingereza’.

Katika shairi la ‘ Kiswahili mama’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Kiswahili ndiye mama, nchini Tanzania’.

Katika shairi la ‘Heko Kawawa mkuza’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Heko Kawawa mkuza, wa lugha ya Kiswahili’.

Katika shairi la ‘Kiswahili Tukipambe’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Kiswahili tukipambambe, kwa mapambo kipambike’.

Katika shairi la ‘Mvunja kwao’ mchomozo takriri wa mistari ni

ka shairi la ‘Kiswahili Kipambwe’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Lugha zile tuziponde, na Kiswahili kipambwe’.

Katika shairi la ‘Lugha’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Kusafirisha mawazo, lugha ni chombo cha muhimu’.

Katika shairi la ‘Ushairi’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘ Washairi yatubidi, kuuhami ushairi’.

Katika shairi la ‘Watunga yele’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Nia ya watunga yele, ni kuvunja Kiswahili’.

Katika shairi la ‘Ni’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Sasa mumeamini?’

Katika shairi la ‘Moyo na macho’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘M kuu wa mapotozo, moyo hapa duniani’.

Katika shairi la ‘Shuku’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Shuku haikuhalisi, kutenda mtu mzima’.

Katika shairi la ‘Mjuzi aso kisomo’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Mjuzi anayejua, bila kisomo ni bora’.

Katika shairi la ‘Jitenge’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Kunena kwangu jitenge, maneno yenye kipyangu’.

atika shairi la ‘Aumbaye Huumbaye’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Aumbaye huumbua, asoumba haumbuai’.

Katika shairi la ‘Hili na lile 1’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Mtu mtu kweli Yule, mjua lile na hili’.

Katika shairi la ‘Sumbo’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Wameghumiwa fumbuzi, fumbo la mfumba sumbo’.

Katika shairi la ‘Katua mwezini’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Watu kufika mbingui, imeshatabiriwa’.

Katika shairi la ‘Hili na lile 2’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘wewe umeelimika, waso elimu wakoje? Mshairi anawataka watu waliopata elimu waitumie elimu yao kwa manufaa ya umma (wawe mfano kwa raia ambao hawakusoma)

Katika shairi la ‘ Taasisi 1’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Ni msinji kwa hakika, taasisi maa yakwe’.

Katika shairi la ‘Taasisi 2’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘ Mwanzo ndiyo taasisi, msingi manaye mwanzo’.

Katika shairi la ‘Piga kama mpigaji’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Piga kama mpigaji, usitukane wapiga’.

Katika shairi la ‘Jinga’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Jinga limekwevuka, halino si jnga tena’.

Katika shairi la ‘Msitu’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Msitu una athari, twende kwa uangalifu’.

Katika shairi la ‘Si lazima tundu zima’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘ Si lazima tundu zima, ndege kusitahimili’.

Katika shairi la ‘Kuku’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Kuku mwala nyama yangu, kinyesi mwachukia’.

Katika shairi la ‘Kunguru’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Kunguru wapo vitani, vindinidi bahati yao’.

Katika shairi la ‘Nyoka mbito’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Aheri ya wote nyoka, kulikoni nyoka mbito’.

Katika shairi la ‘Kidau’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘ Kidau chapepesuka, kimekatika nangaye’.

Katika shairi la ‘Umbea’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘ Si kitu cha kupeneza, umbea unaharibu’.

Katika shairi la ‘Kukinga na kuponya’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Maradhi bora kukuinga, usingojee kuponya’.

Katika shairi la ‘Kujuana’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Utujalie Wadudi, binadamu tujuane’.

Katika shairi la ‘Mghumwa pweke’ mchomozo takriri wa mistari ni ‘Hafoki hapigi ngui, mghumwa pweke halili’.

Katika shairi la ‘Ahadi’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘ Kwa binadamu lawama, kwa Mungu radaye moto’.

Katika shairi la ‘ Ulimwengu’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Katika shairi la ‘Kutowa’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘ Si utajiri kata, katika kutowa kitu’.

Katika shairi la ‘Moyo na macho’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘Mkuu wa mapotozo, moyo hapa duniani’.

Katika shairi la ‘Wema’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘Wema ni kitu buruji, popote ni muuangazo’.

Katika shairi la ‘ Dini’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘ Dini ajali kifaya, faradhi zake Rabia’.

Katika shairi la ‘Lazima alipe shari’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘ Lazima alipwe shari, kila atendaye wema’.

Katika shairi la ‘ Ai gharibi ya Ria’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘ Ai ni sumu ya wenzi, penzi kwa mtu ajabi’.

Katika shairi la ‘ Pendo la pesa’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘ Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo’.

Katika shairi la ‘ Kimada’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘Kimada kakosa haki, kwani si wandoa kamili’.

Katika shairi la ‘Ya allahu ya Robati’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘Likampate Robati, fukisho la manukato’.

Katika shairi la ‘Kimefiwa Kiswahili’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mistari, kwa mfano ‘ Kimefiwa Kiswahili, kufa Bwana Mathias’.

#### **4.2.1.3 Mchomozo Takriri Irabu**

Wamitila , anaeleza kuwa, urudiaji unaopatikana hapa kimsingi ni urudiaji wa kisauti. Takriri irabu hutokea pale ambapo sauti inayorudiwa au kukaririwa ni irabu.

Naye,Mbunda , anasema kuwa, ni marudiorudio ya irabu karibu kila neno. Kwa mfano katika msitari wa kwanza peke yake kuna takriri irabu za “a” “e”, “I” na “u”.

Katika Diwani ya Ustadh Andanenga, mwandishi ametumia mchomozo takriri irabu mfano wake ni; ‘a’ katika shairi la ‘Haki ya kupiga kula’ , ‘Awazalo binadamu’, ‘ Kujitegemea’, ‘ Mapinduzi’, ‘Mwenge’, ‘ Viapo’,’ Kazaliwa Mkombozi’, ‘Lugha’, ‘Kuku’, ‘ Punda’,’Kidau’, Dini’, ‘ na Azimio la Arusha’.

Na, shairi ‘Viapo’ limetumia mchomozo takriri Irabu ‘o’, kwa mfano;

*Mungu walai walao,  
Ni tendo lenye pashao,  
Linatia usambao.*

Mwisho, katika shairi la ‘Ahadi’ ametumia mchomozo takriri Irabu ‘i’ kwa mfano;

*Serikali kuitii,  
Kuasi haifalii’  
Radayo kupigwa zii.*

#### **4.2.1.4 Mchomozo Takriri Vina**

Mbunda, naeleza kuwa, Vina vinavyorudiwarudiwa katika shairi. Hivyo, silabi ambazo hujirudia katika ubeti huweza kujenga takriri vina. Katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*, mchomozo takriri vina umejitokeza katika mashairi mbalimbali, nayo ni kama ifuatavyo:

Katika shairi la ‘Mvunja kwao’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina ‘ni’ katika ubeti wa kwanza na wa pili. Pia, kuna kina cha ‘ma’ katika ubeti wa tatu na wa nne; Na, kuna kina cha ‘bu’ katika shairi hilo la ‘Mvunja kwao’, ubeti wa sita, ubeti wa saba na nane, kuna kina ‘fu’ . Kina ‘a’ ubeti wa tisa, kina ‘ngu’ ubeti wa ‘mu’, kina ‘mbe’ katika ubeti wa kumi na mbili. katika hilo shairi la ‘Mvunja kwao’ katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Haki ya kupiga kura’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, kina ‘ngu’ ubeti wa kwanza, kina ‘ra’ katika ubeti wa pili, kina ‘za’ ubeti wa tatu, kina ‘zi’ ubeti wa nne, kina ‘ya’ ubeti wa tano, kina ‘ma’ ubeti wa sita, kina ‘nda’ ubeti wa saba, kina ‘s’ ubeti wa nane, kina ‘mu’ ubeti wa tisa nawa kumi na moja na kina ‘po’ ubeti wa kumi, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Azimio la Arusha’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina,



mfano kina ‘na’ubeti wa kwanza, kina ‘a’ ubeti wa pili na sita, kina ‘tu’ ubeti wa tatu na nne, kina ‘sa’ ubeti wa tano, kina ‘li’ ubeti wa saba. Katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Tusifu Utamaduni ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘ke’ ubeti wa kwanza, kina ‘ka’ ubeti wa pili na tatu, kina ‘ma’ ubeti wane, kina ‘sha’ ubeti wa tano, kina ‘za’ ubeti wa sita, kina ‘mba’ ubeti wa saba, kina ‘li’ ubeti wa nane na tisa, kina ‘le’ ubeti wa kumi, kina ‘ri’ ubeti wa kumi na moja na kina ‘nga’ ubeti wa kumi na mbili katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Ujengeji wa Taifa ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, kwa mfano kina ‘ra’ ubeti wa kwanza na wa nne, kina ‘zi’ ubeti wa pili, kina ‘tu’ ubeti wa tatu, kina ‘ma’ ubeti wa tano na kina ‘chwa’ ubeti wa sita. Katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Jaribu Tukijaribu ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘wa’ ubeti wa kwanza hadi wa tisa. Katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Uchumi ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘ma’ katika ubeti wa kwanza hadi wa kumi na mbili, kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Awezalo Binadamu ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina ,

mfano kina ‘nga’ ubeti wa kwanza, kina ‘zi’ ubeti wa pili, kina ‘a’ ubeti wa tatu, kina ‘lu’ ubeti wa nne, kina ‘di’ ubeti wa tano na nane, kina ‘ma’ ubeti wa sita , kina ‘la’ ubeti wa saba, kina ‘lo’ ubeti watisa na kina ‘ze’ ubeti wa kumi nan ne, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Katika Kujenge Nchi ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina ,mfano kina ‘wa’ ubeti wa kwanza, kina ‘nde’ ubeti wa pili, kina ‘na’ ubeti wa tatu, kina ‘e’ ubeti wa nne, kina ‘she’ ubeti wa sita, kina ‘o’ ubeti saba, kina ‘mba’ ubeti wa nane na kina ‘ne’ ubeti wa tisa, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘ Kujitegemea’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘nu’ ubeti wa kwanza, kina ‘po’ ubeti wa pili, kina ‘a’ ubeti wa tatu, kina ‘zwa’ ubeti wa nne, kina ‘ke’ ubeti wa sita, kina ‘sa’ ubeti wa saba, kina ‘o’ ubeti wa nane, kina ‘di’ ubeti wa tisa, kina ‘tu’ ubeti wa kumi na kina ‘nda’ ubeti wa kumi na moja, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Mapinduzi ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, kwa mfano, kina ‘mu’ ubeti wa kwanza, kina ‘ma’ ubeti wa pili, kina ‘li’ ubeti wa tatu, kina ‘a’ ubeti wa nne, kina ‘ki’ ubeti wa tano na kina ‘sho’ ubeti wa sita, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Mwenge ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina , mfano kina ‘ sha’ ubeti wa kwanza, kina ‘chi’ ubeti wa pili, kina ‘shwa’ ubeti wa tatu, kina ‘ji’

ubeti wa nne, kina ‘ndo’ ubeti wa tano, kina ‘ja’ ubeti wa sita, kina ‘wa’ ubeti wa saba na kina ‘ma’ ubeti wa nane, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Nchi za watu weusi’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘si’ ubeti wa ubeti wa kwanza hadi wa mwisho, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Tuiunde nchi yetu’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘tu’ katika ubeti wa kwanza hadi wa mwisho, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha Katika shairi la ‘ ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina ‘ ’ katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Ushirika’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘zi’ katika ubeti wa kwanza na wa tano, kina ‘ji’ ubeti wa pili, kina ‘ja’ katika ubeti wa tatu, kina ‘la’ ubeti wa nne, kina ‘ka’ ubeti wa sita, kina ‘ma’ ubeti wasaba na kina ‘ne’ ubeti wa nane, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Kitangazwe Kiswahili’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘za’ katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika kwenye ubeti wa kwanza hadi wa mwisho.

Katika shairi la ‘Kiswahili’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano

kina ‘mbwe’ katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika, kwenye ubeti wa kwanza hadi wa mwisho.

Katika shairi la ‘Watunga yele ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina ,mfano kina ‘li’ katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Moyo na Macho 1 na 2’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘ni’ kimetumiwa kwa beti zote, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Shuku ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina , mfano kina ‘ma’ kwa beti zote, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Piga kama Mpigaji’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘ga’ ubeti wa kwanza hadi wa mwisho, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Si lazima tundu zima ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina , mfano kina ‘li’ kimetumika ubeti wa kwanza hadi wa mwisho, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘ Kuku’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina , mfano kina ‘a’ kimejitokeza katika beti zote, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘ Nyoka mbito ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano

kina ‘to’ kimejitokeza katika beti zote, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Umbea ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘bu’ kimejitokeza kwenye beti zote ,ili katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘ Kujwana ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘ne’ kimejitokeza kwa kila ubeti ili katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Kutowa ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina , mfano kina ‘tu’ kimejitokeza kwa kila ubeti ili katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘ Wema’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina , mfano ‘zo’ ubeti wa kwanza hadi wa mwisho, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Ai ghalibi ya Rai ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina, mfano kina ‘bi’ katika ubeti wa kwanza hadi wa mwisho, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘ Ya Allahu ya Robati ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri

vina,mfano kina ‘to’ kimejitokeza katika beti zote il katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

Katika shairi la ‘Molina tupe nguvuzo ’ mwandishi ametumia mchomozo takriri vina , mfano kina ‘zo’ kimejitokeza katika beti zote kumi na mbili, katika kuonesha msisitizo, ili kufiksha ujumbe wa matini husika.

#### **4.2.1.5 MchomozoTakriri Kituo**

Mbunda (2010) anaeleza kuwa,mshairi amerudia kituo kilekile kutoka ubeti hadi ubeti. Hivyo, kile kituo kinachorudiwa kila ubeti huitwa Takriri Kituo.

Msanii wa *Diwani ya Ustadh Andanenga* ametumia kituo kile kile kwa baadhi ya mashairi na mashairi mengine ametumia kituo kinachobadilika katika mashairi mbalimbali. Kwa mfano;

Katika mashairi yafuatayo, mtunzi ametumia mchomozo takriri kituo ; shairi la ‘ Mvunja kwao’ Takriri kituo ni ‘M vunja kwao ni jura, muradi hana thamani’, shairi la ‘Haki ya kupiga kura’, Takriri kituo ni ‘ Tusipuuze raia, haki ya kupiga kura’, shairi la ‘Azimio la Arusha’ Takriri kituo ni ‘Safari tumeazimu, kwenda kwenye Ujamaa, shairi la ‘Tusifu Utamaduni’ Takriri kituo ni ‘Tusifu utamaduni, wetu wa Kiafrika’, shairi la ‘ Ujengaji wa Taifa’ Takriri kituo ni ‘ Taifa litajengeka ,kwa bidii ya wakazi’, shairi la ‘Jaribu tukijaribu’ Takriri kituo ni ‘Jaribu tukijaribu, kweli tutafanikiwa’, shairi la ‘Uchumi’ Takriri kituo ni ‘Uchumi ni biashara, viwanda na ukulima, shairi la ‘Awezalo Binadamu’, Takriri kituo ni ‘ Awezalo binadamu,

tusiseme hatuwezi’, shairi la ‘ Katika kujenga nchi’, Takriri kituo ni ‘Katika kujenga nchi, tusingoje kutendewa’ na shairi la ‘ Mapinduzi’, Takriri kituo ni ‘Maana ya mapinduzi ni kutafuta hali njema’.

Pia, kuna baadhi ya mashairi ambayo hayajatumia mchomozo takriri kituo na badala yake yana vituo visivyobadilika. Mfano wa mashairi hayo ni ‘Tungo zenu’, ‘ Mdosodo’, ‘Punda’, ‘ Usia’, ‘ Fanya ulizio’, ‘Sauti ya kiza’, ‘ Tumkumbuke Abedi’, ‘ Kwa kifo cha Mathias’, ‘Zamani haiji’ na shairi la ‘ Molina tupe nguvuzo’.

#### **4.2.1.6 Mchomozo Takriri Mizani/ Silabi**

Mbunda (2010) anaeleza kuwa, takriri silabi/ mizani ni kulingana kwa silabi katika kila shairi. Shairi linapotumia mizani kumi na sita katika kila mstari. Kwa hali hiyo tunasema kuna takriri-mizani katika miastari hiyo.

Mashairi yote yametumia mizani kumi na sita ; Mashairi yaliyotumia mizani 16 yako jumla 72 na mfano wa mizani ;kwa mfano, shairi la ‘ Haki ya kupiga kura’, anasema;

‘Le/o/ ma/ku/su/di/ ya/ngu/, na/ta/ka/ ku/si/mu/li/a/’= mizani 16

Ka/ma/ we/ma/ u/nge/li/pwa/, si/ni/nge/i/twa/ fa/ki/ri/ = mizani 16 kaika shairi la ‘Lazima alipe shari’. Mizani katika shairi la ‘Tusifu Utamaduni’ mfano; /Tu / si/ fu/ u/ ta/ma /du /ni /we /tu /wa /Ki /a /f /ri /ka / = Mizani 16

Mizani katika shairi la Azimio la Arusha ‘ mfano; /Ni /na /ni /a /na /ye /gu /na / mbe/ le/ ya/ si/ si/ ka/ u/ mu/ = mizani 16

Mizani katika shairi la ‘Mvunja kwao’ mfano; /M/vu/nja/ kwa/o/ ni/ ju/ra/, mu/ra/di/ ha/na/ tha/ma/ni/= Mizani 16

Katika shairi la ‘Lugha’ mchomozo takriri mizani ni, ‘Ku/sa/fi/ri/sha/ ma/wa/zo/, lu/gha/ ni/ cho/mbo/ cha/ mu/hi/mu’/= mizani 16.

Katika shairi la ‘Ushairi’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘ Wa/sha/i/ri/ ya/tu/bi/di/, ku/u/ha/m/i u/sha/i/ri’.

Katika shairi la ‘Watunga yele’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘Ni/a/ ya/ wa/tu/nga/ ye/le/, ni/ ku/vu/nja/ Ki/swa/hi/li’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Moyo na macho’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘M/ ku/u/ wa/ ma/po/to/zo/, mo/yo/ ha/pa/ du/ni/a/ni’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Shuku’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘Shu/ku/ ha/i/ku/ha/li/si/, ku/te/nda/ m/tu/ m/zi/ma’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Mjuzi aso kisomo’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘M/ju/zi/ a/na/ye/ju/a/, bi/la/ ki/so/mo/ ni/ bo/ra’=mizani 16.

Katika shairi la ‘Jitenge’ mchomozo takriri wa mizani ni ‘Ku/ne/na/ kwa/ngu/ ji/te/nge/, ma/ne/no/ ye/nye/ ki/pya/ngu’= mizani 16.

atikati shairi la ‘Aumbaye Huumbaye’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘A/u/mba/ye/ hu/u/mbu/a/, a/so/u/mba/ ha/u/mbu/a’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Hili na lile 1’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘M/tu/ m/tu/kwe/li/ yu/le/, m/ju/a/ li/le/ na/ hi/li’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Sumbo’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘Wa/me/ghu/mi/wa/ fu/mbu/zi/, fu/mbo/ la/ m/fu/mba/ su/mbo’/ = mizani 16.

Katika shairi la ‘Katua mwezini’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘ Wa/tu/ ku/fi/ka/ mbi/ngu/i/, i/me/sha/ta/bi/ri/wa’/= mizani 16.



Katika shairi la ‘Hili na lile 2’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘we/we/ u/me/e/li/mi/ka/, wa/so/ e/li/mu/ wa/ko/je?/ mizani 16. Mshairi anawataka watu waliopata elimu waitumie elimu yao kwa manufaa ya umma ( wawe mfano kwa raia ambao hawakusoma)

Katika shairi la ‘ Taasisi 1’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘Ni/ m/si/nji/ kwa/ ha/ki/ka/, ta/a/si/si/ ma/a /ya/kwe’/ mizani 16.

Katika shairi la ‘Taasisi 2’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘ Mwa/nzo/ ndi/yo/ ta/a/si/si/, m/si/ngi/ ma/na/ye/ mwa/nzo’/ = mizani 16.

Katika shairi la ‘Piga kama mpigaji’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘Pi/ga/ ka/ma/ m/pi/ga/ji/, u/si/tu/ka/ne/ wa/pi/ga’/= mizani 16.

Katika shairi la ‘Jinga’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘Ji/nga/ li/me/kwe/vu/ka/, ha/li/no/ si/ ji/nga/ te/na’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Msitu’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘ M/si/tu/ u/na/ a/tha/ri/, twe/nde/ kwa/ u/a/nga/li/fu’/= mizani 16.

Katika shairi la ‘Si lazima tundu zima’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘ Si/ la/zi/ma/ tu/ndu/ zi/ma/, nde/ge/ ku/si/ta/hi/mi/li’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Kuku’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘Ku/ku/ mwa/la/ nya/ma/ ya/ngu/, ki/nye/si/ mwa/chu/ki/a’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Kunguru’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘Ku/ngu/ru/ wa/po/ vi/ta/ni/, vi/ndi/ni/di/ ba/ha/ti/ ya/o’/mizani 16.

Katika shairi la ‘Nyoka mbito’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘A/he/ri/ ya/ wo/te/ nyo/ka/, ku/li/ko/ni/ nyo/ka/ mbi/to’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Kidau’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘ Ki/da/u/ cha/pe/pe/su/ka/, ki/me/ka/ti/ka/ na/nga/ye’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Umbea’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘Si/ ki/tu/ cha/ ku/pe/ne/za/, u/mbe/a /u/na/ha/ri/bu/’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Kukinga na kuponya’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘Ma/ra/dhi/ bo/ra/ ku/ku/i/nga/, u/si/ngo/je/e / ku/po/nya/’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Kujuana’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘U/tu/ja/li/e/ Wa/du/di/, bi/na/da/mu/ tu/ju/a/ne/’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Mghumwa pweke’ mchomozo takriri wa mizani ni, ‘Ha/fo/ki/ ha/pi/gi/ ngu/i/, m/ghu/mwa/ pwe/ke/ ha/li/li/’= mizani 16.

Katika shairi la ‘ Ahadi’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mizani, kwa mfano ‘ Kwa/ bi/na/da/mu/ la/wa/ma/, kwa/ Mu/ngu/ ra/da/ye/ mo/to/’= mizani 16.

Katika shairi la ‘ Ulimwengu’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mizani, kwa mfano ‘Cha/ we/nye/ ra/ha/ na/ ta/bu/, u/li/mwe/ngu/ ni/ ki/wa/nja/’.= mizani 16

Katika shairi la ‘Kutowa’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mizani, kwa mfano ‘ Si/ u/ta/ji/ri/ ka/ta/, ka/ti/ka/ ku/to/wa/ ki/tu/’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Moyo na macho’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mizani, kwa mfano ‘ M/ku/u/ wa/ ma/po/to/zo/, mo/yo/ ha/pa/ du/ni/a/ni/’= mizani 16.

Katika shairi la ‘Wema’ mwandishi ametumia mchomozo takriri mizani, kwa mfano ‘ We/ma/ ni/ ki/tu/ bu/ru/ji/, po/po/te/ ni/ mu/u/a/nga/zo/’= mizani 16.

Pia, kuna baadhi ya mashairi ambayo yametumia mizani pungufu ya kumi na sita.

Mfano wa mashairi hayo ni ‘Fanya ulizio’ anasema,

Le/o/ ni/na/ ja/mbo/, na/ta/ka/ ku/kwa/mbi/a= mizani 12

Na shairi la ‘ Sauti ya kiza’ mizani yake ni,

Nga/ku/a/ na/ ma/to/, ya/ ku/o/ne/a= mizani 11.

#### 4.2.1.7 Mchomozo Takriri Konsonanti

Mbunda (2010) anasema kuwa, Marudiorudio ya Konsonanti pia yapo, ambayo hujitokeza katika urudiwaji wa konsonanti katika msitari au ubeti na katika shairi zima. Nayo yanafanana na marudiorudio ya irabu.

Katika shairi la ‘Mvunja kwao’ Kwa mfano katika ubeti wa tatu kuna mchomozo takriri konsonanti “k” au “h”...Takriri hizo za konsonanti zimeenea katika shairi zima. Kwa mfano;

*Hathamini kwa thama, hata kama akipura  
Hata kama kasimama, katikati ya kinara  
Lile atalolisema, katu halipati kura*

Mfano mwingine wa mchomozo takriri konsonanti ni katika shairi la ‘Pendo la pesa’, kuna urudiwaji wa konsonanti “P” na “h” katika ubeti wa pili. Kwa mfano,

*Pendo halina utamu, lina harufu jamee  
Pendo ninalilaumu, mimi lisiinilemee  
Pendo halina kudumu, hadi pesa umwekee  
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.*

#### 4.2.1.8 Mchomozo Takriri Muundo

Mbunda (2010) ni utumizi wa mishorooro na mizani yenye ulingano kwa kila ubeti katika shairi.

Katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*, mtunzi ametumia mchomozo takriri muundo, ambapo, muundo wa mashairi mengi pia unarudiwa kutoka ubeti hadi ubeti. Kwa mfano katika shairi la ‘Tuiunde nchi yetu’ mshairi anasema;

*Tuiunde nchi yetu, shime tuondoe chuki  
Tumwombe kwa Barakatu, aziondoe fatiki*

*Atupe nyoyo za utu, sio zile za nyamaki  
Shime tuondoe chuki, tuiunde nchi yetu.*

Pia, katika shairi la ‘Punda’ muundo huo pia umetumika, kwa mfano;

*Mwana ushike usia, kabla chini sijaenda  
Yapasa kuzingatia, usiwe kama mkanda  
Baada ya kufungia, hapo basi umegenda  
Wa madhehebu ya punda, yafaa kumkiuka.*

Tumetumia mifano michache hiyo kuonesha mchomozo takriri muundo ambao mwandishi ameutumia, kwa vile kuandika mifano yote ndani ya diwani ni sawa na kunakili kitabu chote kizima.

#### **4.2.1.9 Mchomozo Takriri Ridhimu**

Mbunda (2010) anaeleza kuwa, Ridhimu ni mapigo katika shairi au wimbo. Hayo mapigo asilia kwa kawaida kila lugha ina mapigo yake. Ina mawimbi ya kupanda na kushuka na kwa kawaida mawimbi hayo huambatana na maana. Mshairi wa *Diwani ya Andanenga*, ametumia pia, mchomozo takriri ridhimu katika mashairi yake yote. Hapa, tumetoa mfano wa beti mbili ili kuonesha uridhimu uliomo katika kila ubeti.

Kwa mfano, katika shairi la ‘Punda’ mwandishi, anasema;

*Mwa-na- u-shi-ke- u-si-a-, ka-b-la- chi-ni- si-ja-e-nda,  
Ya-pa-sa- ku-zi-nga-ti-a-, u-si-we- ka-ma- m-ka-nda,  
Ba-a-da -ya -ku-fu-ngi-a-, -ha-po -ba-si -u-me-ge-nda,  
Wa- ma-dhe-he-bu- ya- pu-nda-, ya-fa-a -ku-m-ki-u-ka.*

Na, mfano wa pili ni katika ushairi wa ‘Pendo la pesa’ mshairi anasema;

*Pe-ndo- ha-li-na- u-ta-mu-, li-na- ha-ru-fu- ja-me-e,  
Pen-do -ni-na-li-la-u-mu-, -mi-mi -li-si-nil-e-me-e,  
Pe-ndo- ha-li-na- ku-du-mu-, ha-di- pe-sa- u-mwe-ke-e,  
Pe-ndo- ha-li-na- she-re-e-, pe-ndo- la- pe-sa- si- pe-ndo.*

#### 4.2.1.10 Mchomozo Takriri Mawazo

Mbunda (2010) anaeleza kuwa, Mshairi anayerudia mawazo yaleyale kutoka ubeti hadi ubeti, ingawa pengine huleta wazo jipya. Takriri zote hizi hujenga taathira maalumu zinazoleta hisia Fulani.

Katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*, mchomozo takriri mawazo, umetumika katika mashairi mbalimbali. Mfano katika shairi la ‘Pendo la pesa’ katika ule ubeti wa kwanza na ule wa tano kuna mchomozo takriri mawazo, ambao umejitokeza. Mfano wake ni huu ufuatao;

*Pendo la pesa si pendo, mbali nalo jitenge  
Pendo lanuka uvundo, mbali nail jitenge  
Pendo halina uhondo, katu usilichekee  
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.*

*Pendo kutumia hela, mifuko iteketee  
Pendo hilo lahaula, ni zigo ujibebeee  
Pendo wawili ni kula, nyama ndimi mnene  
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo*

Mawazo katika beti zote hizo mbili ni juu ya kujitenga na kuepuka mapenzi yanayotumia pesa. Katika ubeti wa pili hapo ni msisitizo wa ubeti wa kwanza. Mwandishi ameonesha hasara za mapezi yasiyoongozwa na upendo wa moyoni kwani huwa hayadumu na yanaweza kusababisha ugonjwa hata kusababisha kifo kwa wahusika. Tuangalie ubeti ufuatao;

*Pendo hapa nakomesha, mbele nisiendeleee  
Pendo la pesa lafisha, ni gonjwa usipokee  
Pendo hadhi linafisha, la pesa sipendeleee  
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.*

Tuangalie mfano ufuatao tena katika shairi la ‘Kaziliwa mkombozi’, ambo dhana ya mchomozo takriri mawazo umejitokeza katika ubeti wa pili na ubeti wa nane. Kwa mfano;

*Wa kondoo wapotevu, kazaliwa mkombozi  
Yesu mwondoa maovu, dhambi ni kila ajizi  
Hujenga maelekevu, hutatua matatizi  
Kaziliwa mkombozi, wa kondoo wapotevu.*

Wazo linaloongelewa na mwandishi hapo ni kwamba, lengo la kuzaliwa kwa Yesu hapa duniani ni kuwaokoa wanadamu na kuondoa maovu na dhambi zetu wanadamu ili waishi kwa amani. Lakin vilevile katika ubeti wa nane ameleza kuwa Yesu mkombozi kaleta usuluhivi/ amani nani kiongozi bora.

*Wa kondoo wapotevu, ndiye mimi mtengezi  
Naleta usuluhivu, pamoja na uongozi  
Sitatumia mabavu, Baba kanipa ujuzi  
Kaziliwa mkombozi, wa kondoo wapotevu.*

Ubeti huu umetuonesha faida zaidi ya kuzaliwa Mkombozo ambapo, yeye ni kiongozi, kaleta suluhu na sisi tunamtegemea daima. Hivyo wazo ni lile lile ila kwa hapa linapanuliwa zaidi.

Dhima ya matumizi ya mchomozo takriri na aina zake ni pamoja na kupamba lugha, kuelekeza mwendo wa shairi, kisisitiza ujumbe na kufurahisha wasomaji.

#### **4.2.2 Mchomozo Ukengeushi/ Ukiushi**

Jilala (2016) anaeleza kuwa, ukengeushi ni hali ya kutumia kaida tofauti ama kinyume na jinsi ilivyozoeleka katika utunzi ama uwasilishaji wa kazi za fasihi. Hii inamaana kwamba, ukiushi ni ukiukaji wa kanuni ama mazoea.

Katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*, mchomozo ukengeushi umejitokeza katika sehemu mbalimbali. Kwa mfano: Katika shairi la ‘Mvunja kwao’ katika ubeti wa tano mshororo wa pili na ubeti wa saba mshororo wa kwanza na wa pili, anasema;

*Hapati rafiki mwema, kuunga yake dharma  
Hapewi habari njema, palipo watu duara  
Wota watamsukuma, au kupigwa bakora  
Mvunja kwao ni jura, muradi hana thamani.*

*Hana thamani ya dafu, au ni ya moja pera  
Si thamani ya mkufu, thamaniye ni kangara  
Yenye wingi wa harufu, mnywaji huwa papara  
Mvunja kwao ni jura, muradi hana thamani.*

Katika shairi la ‘Mvunja kwao’ maneno kama ‘watu dura’ ni ukengeushi wa watu wenye tabia mbaya, kwani kwa kawaida hatuna watu wenye umbo la duara. Pia, thamani ya mtu kulinganishwa na dafu na pera, kisha kufananishwa na kangara ni ukengeushi. Thamani ya binadamu ni kubwa kuliko vitu vyote.

Katika shairi la ‘Tuiunde nchi yetu’ kuna ukengeushi ambao umejitokeza katika ubeti wa tatu na ule mshororo wa kwanza. Mwandishi, anasema;

*Mungu tuondoe kutu, wote tuwe marafikai  
Wema mpe kila mtu, utujazie Awaki,  
Kiumbacho Haifatu, kipe mema kimiliki  
Shime tuondoe chuki, tuiunde nchi yetu.*

Ukengeushi uliojitokeza ni ‘Mungu tuondoe kutu’ kutu hutokea pale chuma kinapokutana na maji. Mwandishi ametumia kutu akimaanisha roho mbaya. Kutu ni ukengeushi kwani watu hatuoti kutu daima.

Katika shairi la ‘Dhamiti ya nchi yetu’ mwandishi ametumia ukengeushi katika ubeti wa kwanza na mshororo wa tatu. Neno macho ‘kwatua kwatua’ ni ukengeushi wa fumbua macho uangalie au utazame. Mwandishi anasema,

*‘Na macho kwatua kwatu, usikilize ya bashasha’*

Vilevile katika shairi la ‘Heko Kawawa mkuza’, mchomozo ukengeushi umejitokeza katika ubeti wa tano, mshororo ule wakwanza. Neno ‘Kugaragara’ ni ukengeushi wa

kupuuzwa au kudharauliwa. Kwa kawaida lugha ni kitu ambacho hakishikiki, hivyo hakiwezi kugaragazwa. Pia neno ‘kikikabwa’ nalo ni ukengeushi wa kunyimwa nafasi. Mwandishi anasema;

*‘Kiswahili kikikabwa, juani kugaragara’*

Katika shairi la ‘ Kiswahili tukipambe’, mchomozo ukengeushi uliojitokeza ni katika ubeti was aba na ule mshororo wa pili na tatu. Mwandishi anasema;

*Yawe makali ya kisu, ama kulikoni wembe  
Kiswahili tukibusu, kwa ndimi zetu tulambe*

Mashairi kuwa na makali ya wembe au kisu ni ukengeushi wa maudhui ya ushairi yalenge mahitaji ya jamii na yawafunze watu wabadilike. Wakati Kiswahili tukibusu ni ukengeushi wa lugha ya Kiswahili tuipele na kuitumia kila wakati.

Katika shairi la ‘ Shuku’ msanii ametumia mchomozo ukengeushi katika ubeti wa kumi na moja mshororo wa kwanza, ambapo shuku ameita ni nyama ya fisi. Akimaanisha kuwa shuku ni mbaya haifai kuwepo miongoni mwa wanajamii, kwani hata nyama ya fisi huwa hailiwi na watu ndivyo hivyo na shuku , yaani hali ya kutokuaminiana miongoni mwa wanajamii haitakiwi.

*‘Hailiwi ni haramu, shuku ni nyama ya fisi’.*

Katika shairi ya ‘Punda’, mwandishi ametumia mchomozo ukengeushi kufikisha ujumbe kwa jamii ili iachane na tabia ambazo siyo nzuri katika jamii. Kwa mfano , anasema wa madhehebu ya punda, chui, paka, samba na tumbili, yafaa kujitenga nao. Anachokimaanisha ni kwamba watu wenye tabia ambazo siyo nzuri hawafai kuwa rafiki zetu, tujitenge nao.



Na katika shairi la ‘Tumkumbuke Abedi’ katika ubeti wa tatu, mshororo wa nne, mwandishi ametumia neno ‘ametika’ ikiwa ni ukengeushi wa kufa ya Mwenyezi Mungu amemuita naya akaitika ( kufa). Ujumbe anaoutoa hapa ni kwamba hakuna kiumbe muweza kama Mungu, hivyo tumche yeye kabla hajatuita. Mwandishi anasema;

*‘Ameitika Abedi, mlezi wa lugha yetu’.*

Utafiti huu umechunguza mdafao wa ujitokezaji wa vipengele vya mchomozo katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*. Matokeo yalikuwa yanaonekana katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na 4.1: Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Mchomozo kwa ujumla**

Aina	Mdafao		%
Mchomozo Takriri	Neno	219	0.43
	Mistari	557	1.11
	Irabu	339	0.67
	Vina	2688	5.36
	Kituo	557	1.11
	Mzani / Silabi	43012	85.79
	Konsonanti	48	0.09
	Muundo	4	0.00
	Ridhimu	2688	5.36
	Mawazo	10	0.01
Ukengeushi		11	0.02
Jumla		50133	100

Chanzo: Mtafiti (2016)

#### **4.3 Kulinganua na Kulinganisha Uteuzi wa Mbinu za Mchomozo katika Diwani ya Ustadh Andanenga**

*Jilala (2016:140) anasema, ‘Mwanafasihi linganishi analinganisha vipengele vya fani na maudhui alivyovibainisha katika hatua ya*

*uchambuzi...anatakiwa kueleza sababu ya kufanana na kutofautiana kwa kazi hizo na kuonesha ushahidi wa kisayansi unaothibitisha kufanana ama kutokufanana kwa kazi hizo'.*

Na sisi katika ulinganishaji wetu wa Mchomozo na vipengele vyake tumezingatia maelezo ya Jilala. Utafiti huu umechambua na kuchunguza mchomozo na vipengele vyake vilivyotumika katika *Diwani ya Ustadh Andanengaili* kuona ni jinsi gani msanii wa diwani hiyo ametumia mchomozo. Je, kuna kufanana ama kutofautiana katika uteuzi wa mbinu za vipengele vya mchomozo katika matini? Matokeo ya utafiti huu yalikuwa kama yalivyowasilishwa katika vipengele vifuatavyo.

#### **4.3.1 Kutofautiana**

Katika uchunguzi wetu, utafiti huu umebaini kuwa, msanii ametumia vipengele vya mchomozo kwa namna tofauti na uteuzi wa mbinu hizo unatofautiana kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano, imebainika kuwa katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*, msanii ametumia zaidi kipengele cha Mchomozo Takriri kwa asilimia 99.93% na Mchomozo Ukengeushi kwa asilimia 0.02%.

Na ujitokezaji wa vipengele vya Mchomozo Takriri ni kwamba; kipengele cha mchomozo takriri silabi/ mizani kimejitokeza zaidi kwa asilimia 85.79%, kipengele cha mchomozo takriri vina na mchomozo takriri ridhimu vimejitokeza kwa asilimia 5.36% kila kimoja. Vipengele vya mchomozo takriri mistari na mchomozo takriri kituo navyo kila kimoja kimejitokeza kwa asilimia 1.11%, kipengele cha takriri neno kimejitokeza kwa asilimia 0.43%, takriri irabu kwa asilimia 0.67%, takriri konsonanti kwa asilimia 0.09%, takriri mawazo/ wazo kwa asilimia 0.01% na

kipengele cha takriri muundo kimejitokeza kwa asilimia 0.00%. Hii ni kutokana na msanii kutumia miundo ya aina tatu tu.

#### **4.3.2 Kufanana**

Katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*, kuna vipengele baadhi ambavyo vimejitokeza katika hali ya kufanana kwa asilimia. Kwa mfano kipengele cha mchomozo takriri mistari kimejitokeza kwa asilimia 1.11% sawa sawa na kipengele cha mchomozo takriri kituo ambacho nacho kimejitokeza kwa asilimia 1.11%. Pia, kipengele cha mchomozo takriri vina kimejitokeza kwa asilimia 5.36% sawa sawa na kipengele cha mchomozo takriri ridhimu ambacho nacho kimejitokeza kwa asilimia 5.36%.

#### **4.4 Sababu za Kufanana Na Kutokufanana**

Ikumbukwe kwamba , takriri mistari ni ule ujirudiaji wa mshororo mmoja katika kila ubeti wa ushairi. Mara nyingi ujirudiaji huo wa mshororo hujitokeza katika kila mstari wa mwisho wa kila ubeti na hivyo, kusababisha dhana ya takriri mistari kufanana na ile ya takriri kituo. Kwani takriri kituo ni ule ujirudiaji wa mshororo wa mwisho kwa kila ubeti. Kwasababu hizo na maelezo hayo hapo juu takriri mistari na takriri kituo vimejitokeza kwa asilimia 1.11% kila kimoja.

Vipengele vingine ambavyo vimefanana ni kipengele cha takriri vina na takriri ridhimu. Takriri kina ni ule ujirudiaji wa sauti, ambazo hujitokeza katika ya ubeti na mwishoni mwa ubeti wa shairi. Na, takriri ridhimu ni mapigo ya kupanda na kushuka kwa sauti katika ushairi. Mara nyingi ridhimu hujitokeza katika kina cha kati na kila cha mwisho. Hivyo ndiyo sababu ya kufanan kwa kipengele cha takriri vina na takriri ridhimu, ambavyo vimejitokeza kwa asilimia 5.36% kwa kila kimoja.

Ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilo maalumu wa maneno fasaha na yenye muwala, yaliyoandikwa kwa lugha ya mkato, picha, sitiari au ishara, katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo, ili kuleta wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisia fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo. Ujitokezaji wa vipengele vya mchomozo takriri na mchomozo ukengeushi unatofautiana kutokana na kwamba, ushairi ni kanuni na kanuni hizo ni mpangilio wa maneno, vina, mizani / silabi na ruka ya mkato ambavyo vimeweza zaidi kujitokeza katika mchomozo takriri kuliko mchomozo ukengeushi. Pia, kuna tofauti ujitokezaji wa vipengele vya takriri. Na, kipengele cha takriri silabi / mizani kujitokeza zaidi ya vipengele vingine vya takriri hii ni kutokana na kuwa sifa kubwa ya ushairi ni kanuni ya mizani/ silabi.

#### **4.5 Hitimisho**

Sura hii imewasilisha na kujadili data na matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu kulingana na malengo mahususi ya utafiti kama yalivyobainishwa katika sura yakwanza. Sura hii imebainisha vipengele vya mchomozo ambavyo vimetumika katika diwani iliyochunguzwa katika utafiti huu ambayo ni *Diwani ya Ustadh Andanenga*. Utafiti huu umebaini kuwa *Diwani ya Ustadh Andanenga* imetumia vipengele vya Mchomozo ambavyo ni takriri na ukengeushi. Imejadiliwa katika suara hii kuwa, kipengele chamchomozo takriri kimejitokeza zaidi katika kuwasilisha kazi yake. Wakati katika kipengele cha mchomozo ukengeushi, kipengele hiki diwani hii imetumia kwa kiwango kidogo zaidi katika kufikisha maana ya matini. Sura inayofuata ni sura ya tano, inahusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya tasnifu hii.

## SURA YA TANO

### 4.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni; utangulizi, muhtasari, hitimisho la utafiti huu na sehemu ya nne ni mapendekezo ya utafiti huu.

#### 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ni utafiti linganishi ambao umelinganisha vipengele Mchomozo katika *Diwani Ustadh Andanenga* iliyoandikwa na Amir A. Sudi Andanenga. Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza vipengele vya Mchomozo vilivyojitokeza katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*, ili kubaini vipengele vinavyofanana na kutofautiana katika kuliwasilisha maana ya matini au ujumbe kupitia diwani hii.

Tatizo la utafiti huu ni kutaka kuchunguza vipengele vya mchomozo vilivyojitokeza katika *Diwani ya Ustadh Andanenga* ili kuona ni jinsi gani msanii mmoja wa diwani hiyo anavyo fanananisha ama kutofautisha katika kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Aidha, lengo la utafiti huu kama lilivyobainishwa katika sura ya kwanza ilikuwa ni kubainisha vipengele vya Mchomozo katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*, ili kubaini vipengele vinavyofanana na kutofautiana. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi mawili ambayo ni; (i) Kubainisha vipengele vya mchomozo katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*. (ii) Kulinganua na kutofautisha uteuzi wa vipengele vya Mchomozo katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii. (iii) Kueleza sababu za kufanana na kutofautiana huko.

Ili kufikia malengo hayo, utafiti huu ulikusudia kujibu maswali matatu ambayo ni; Je, ni vipengele vipi vya mchomozo vilivyojitokeza katika *Diwani ya Ustadh Andanenga* Je, uteuzi wa vipengele vya hivyo vya Mchomozo katika *Diwani ya Ustadh Andanenga* vinafanana ama kutofautiana katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii? Je, kufanana na kutofautiana huko kunasababishwa na nini?

Pamoja na kuwa kuna tafiti ambazo zimefanywa kuhusu ushairi na mtindo, lakini ulinganishaji huo haukuzingatia vipengele vya mchomozo katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*. Vile vile tafiti nyingi zimejikita katika kulinganisha fani na maudhui ya kazi za fasihi. Na tafiti hizo hazikuhusisha kazi za mtunzi mmoja. Hivyo, bado ilionesha kuwa utafiti wa kina unahitajika ili kutafiti jinsi vipengele vya mchomozo vinavyoweza kutofautisha msanii mmoja peke yake katika kazi moja, pengo hili ndilo ambalo utafiti huu ulikusudia kuliziba. Ili kufikia lengo na kuziba pengo hilo, utafiti huu basi, ulichunguza vipengele vyamchomozo katika ushairi kwa kutumia mifano ya *Diwani ya Ustadh Andanenga*.

Aidha kulingana na malengo ya utafiti huu, utafiti huu ulitumia nadharia ya Umaksi ambayo ilionekana inafaa na imetuongoza katika kuchunguza na kuchambua data za utafiti huu.

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu moja ambayo ni; (kusoma matini) maktaba. Mbinu ya usomaji wa machapisho ilikuwa ni mbinu kuu ambayo ilimsaidia mtafiti kuchambua na kubainisha vipengele vya mchomozo vinavyotumika kufikisha ujumbe wa kazi ya sanaa. Utafiti huu unatumia sifa za

utafiti wa kitakwimu na usiokitakwimu. Aidha, data ya utafiti huu imechambuliwa kwa kutumia mbinu mbili, yaani uchambuzi maudhui na uchambuzi linganishi.

Katika kujibu maswali ya utafiti huu, kwa kuanza na swali la kwanza, utafiti huu ulichunguza vipengele vya Mchomozo katika *Diwani ya Ustadh Andanengana* kubaini kuwa, msanii ametumia vipengele vya Mchomozo ambavyo ni; takriri na ukengeushi.

Swali la pili la utafiti huu liliweza kujibiwa kwa data zilizopatikana katika utafiti huu kama ifuatavyo. Katika kulinganisha na kulinganua jinsi msanii wa *Diwani ya Ustadh Andanenga* ametumia vipengele vya mchomozo katika kuwasilisha ujumbe. Utafiti huu umebainia kuwa, msanii ametumikia takriri zaidi na hasa katika kipengele cha silabi/ mizanikimejitokeza zaidi. Aidha utafiti huu umebaini kuwa, *Diwani ya Ustadh Andanenga* imesheni mbinu ya mchomozo takriri mbalimbali ambazo zimetumika katika kufikisha dhima ya mtunzi kwa jamii husika, kwani mchomozo takriri silabi /mizani kimejitokeza kwa asilimia 85.79%.

Utafiti huu ulibaini kuwa *Diwani ya Ustadh Andanenga* imetumia kwa kiasi kidogo zaidi kipengele cha mchomozo ukengeushi kwa asilimia 0.02% tu.

Utafiti huu umebainisha pia, kuwa pamoja na ukweli kuwa kuna tofauti finyu baina ya takriri mistari na takriri kituo. Na upo ukaribu wa kidhana na ujitokezaji wa takriri ridhimu na takriri vina. Ndiyo maana vipengele hivi vimejitokeza kwa asilimia 5.36% kila kimoja.

Na mbinu ya mchomozo ni dhana pana inayoweza kueleweka kama dhana ya kipragmatiki inayorejelea usoutuami wa mawasiliano kati ya mwandishi wa matini na msomaji. Matumizi ya mchomozo katika matini husaidia kubainisha kwa haraka kile kilichokusudiwa na mtunzi, kujenga mtindo, muundo wa matini husika na kujenga maana katika matini husika.

Aidha, katika mambo yaliyofanana katika *Diwani ya Ustadh Andanenga* ni kipengele cha takriri kituo na takriri mistari. Ufanano mwingine ni kwamba, vipengele cha takriri ridhimu na takriri vina vimejitokeza kwa asilimia sawa. Utafiti huu umebaini kuwa *Diwani ya Ustadh Andanenga* imeandikwa katika kipindi cha Ukoloni mambo leo ili kuwaelimisha raia waondokane na kasumba ya kuwaabudu Wazungu na kutegemea misaada zaidi. Badala yake msanii anawataka wananchi wajitume katika kazi, waishi kwa amani, wazingatie demokrasia ya kweli na kuwepo na mapenzi ya kweli katika jamii miongoni mwa wanandoa na jamii kwa ujumla.

Mwandishi amewataka watu kuepuka kasumba za kikoloni kwa kudharau lugha ya Kiswahili na kuthamini lugha za kigeni. Msanii amebainisha wazi kuwa watu wanaoidharau lugha ya Kiswahili hao ni watumwa na hawajitambui. Ametushauri kuiga mfano wa Kawawa ambaye alihimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kila Nyanja hapa nchini.

Swali la tatu, ambalo lilitaka kueleza sabaabu za kufanana na kutokufanana, utafiti huu umebaini kuwa, *Diwani ya Ustadh Andanenga*, vipengele vya takriri vina na takriri ridhimu zinafanana kutokana na dhana hizi kufanana katika maana zake na mifano yake. Ufanano mwingine ni ule uliojitokeza katika kipengele cha takriri



mistari na takriri kituo. Pili, sababu za kufanana kwa vipengele hivi ni kutokana na dhana hizi kuingiliana katika maana zake na hivyo kusababisha vipengele hivyo kujitokeza kwa asilimia sawa.

Katika sababu za kutofautiana kwa kipengele cha takriri silabi/ mizani na vipengele vingine ni kwamba, ushairi hutumia maneno yaliyo katika mafungu, ushairi hufuata kanuni za mizani au iddi ya silabi, ndiyo maana silabi/ mizani imejitokeza kwa wingi zaidi.

### **5.3 Hitimisho**

Utafiti huu umejadili kuwa, vipengele viwili vya mchomozo ambavyo ni takriri na ukengeushi, ambavyo vimejitokeza katika diwani iliyochunguzwa katika utafiti huu ambazo ni *Diwani ya Ustadh Andanenga*. Utafiti huu umebaini kuwa Diwani ya Ustadh Andanenga imetumia vipengele vya mchomozo ambavyo ni takriri na ukengeushi. Na vipengele vya takriri, ambavyo ni; takriri neno, takriri mistari, takriri irabu, takriri vina, takriri kituo, takriri silabi, takriri konsonanti, takriri muundo, takriri ridhimu na takriri mawazo. Utafiti huu umebaini kuwa, *Diwani ya Ustadh Andanenga* imetumia zaidi takriri silabi / mizani katika kuwasilisha maana ya matini yake na hivyo kumfanya msomaji aweze kufikiri zaidi ili kuweza kubaini kile msanii alichokusudia. Tofautina kipengele cha ukengeushi ambacho kimetumika kwa kiwango kidogo kwani kingetumika kwa wingi pengine kingesababisha maana ya matini isifike vizuri kwa msomaji wa kazi ya fasihi.

Imejadiliwa kuwa Diwani hii ni matokeo ya nadharia ya Kimaksi (Marx's) kwani

matukio ya utabaka kati ya wenye nacho na wale wasiokuwa nacho, tofauti na utabaka huo miongoni mwa wanajamii ndiyo matokeo ya kazi hii.

Kulingana na utafiti huu, tunaweza kuona faida ya utafiti huu kwa taaluma ya fasihi na jamii kwa ujumla. Kwanza kupitia utafiti huu utachochea ari ya kufanyia utafiti kazi mbalimbali za kifasihi hususani ushairi wa Kiswahili pia katika diwanizinazozungumzia ukoloni mamboleo na matabaka katika jamii.

Pili, kupitia utafiti huu una faida kubwa kwa wasomi kwani utatajirisha maktaba zetu ikiwemo ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambapo wasomi watasoma na kupata rejea ya mambo mbalimbali ya mchomozo katika ushairi na watafiti wengine wakiutumia utafiti huu kwenye kazi zao tangulizi.

Tatu, utafiti huu umesaidia kuongeza maarifa na ufahamu kwani vipengele vya mchomozo ambavyo ni pamoja na takriri na ukengeushi, ambavyo navyo vina vipengele vyake, vilivyofafanuliwa namna vilivyotumika katika kazi hizo za kifasihi. Wale watakao kuwa wanaisoma kazi hii watakuwa wanaongeza maarifa yao juu ya mtindo na vipengele vyake. Nne, utafiti huu umetoa mchango wake kwa jamii kwa kutaka kuonesha umuhimu wa kazi ya ushairi na namna gani kazi mbalimbali za kifasihi hubeba historia ya nchi. Tano, utafiti huu ni muhimu kwa wanafasihi linganishi, kwamba umepanua zaidi wingo wa vipengele vya mchomozo ambavyo ni takriri na ukengeushi, ambapo kipengele cha takriri kina vipengele vyake.

#### **5.4 Mapendekezo**

Kwa kutumia utafiti huu tumeweza kulinganisha ushairi wa kiswahili, utafiti huu

unahitimisha kuwa *Diwani ya Ustadh Andanenga* imewasilisha vipengele vya mchomozo na kipengele cha takriri mizani/ silabi kimejitokeza zaidi. Hivyo basi, utafiti huu unapendekeza kwamba ipo haja ya kufanya utafiti wa kina zaidi kuhusu kazi mbalimbali za kifasihi hasa katika kipengele cha mchomozo na katika takriri ili kubainisha zaidi vipengele vingine vya mchomozo kama vile ushikamani na usambamba, ambavyo utafiti huu haukuvibainisha.

Utafiti mwingine ambao tunapendekeza kwa watafiti wajao ni upande wa mbinu za ushikamani ubadala na aina zake kama urejelezi wa nafsi, mahali na wa karibu, huenda ikapatikana mbinu ya urejelezi mwingine. Kwa kufanya hivi tumeweza kutoa hitimisho la jinsi msanii anavyoweza kutumia ubunifu wa vipengele vyake vya mchomozo katika kuwasilisha ujumbe wa ukoloni mamboleo na mawaidha mbalimbali katika *Diwani ya Ustadh Andanenga*.

### MAREJELEO

- Abdalla, A. (1973). 'Ushairi wa Kiswahili na uhuishwe usiuliwe' Katika zindiko, Dar es Salaam, Chama cha Kiswahili, Chuo kikuu cha D' Salaam, Tanzania.
- Abeid, A. K. (1981). Sheria za kutunga Mashairi na Diwani ya Amri, Mjini Nairobi: Literature Bweru.
- Alderson, C. G. & Beretta, A. (1992). (Wah.) *Evaluating Second Education: Cambridge Applied Linguistics*, Cambridge: Cambridge University Press.
- Bachman, R. & Schutt, R. (2007). *The Practice of Research in Criminology and Criminal Justice* (Toleo la 3). Thousand Oaks, CA: Sage Publications.
- Baker, T. (1994). *Doing Social Research*. Kualar Lumpar: McGraw-Hill.
- Bryman, A. (2004). *Social Research Methods* (Toleo la 2). Oxford: Oxford University Press.
- Christopher, A. S. (h.t). Nadharia na uhakiki wa tamthili ya Christopher AS (h.t) Nadharia, mbinu na mifano ya kazi bunilizi, Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.
- Cooper, H. (1989). *Homework*. New York: Longman.
- Corbetta, P. (2003). *Social Research: Theory, Methods and Techniques*. London: Sage Publications Inc.
- Cuddon, J. A. (1998). *Dictionary of Literarry Terms and Literary Theory*, London: AndreDeutsch.
- Daymon, C. & Holloway, I. (2002). *Qualitative Research Methods in PublicRelations and Marketing Communications*. London: Routledge.
- De Vaus, D. A. (1993). *Surveys in Social Research* (Toleo la 3.). London: UCL Press.

- Eagleton, T. (1983). *Literary Theory: An Introduction*. Cambridge: Blackwell.
- Holloway, L. (1997). *Basic Concepts for Qualitative Research*. Oxford: Blackwell Science.
- Jakobson, R. (1987). *Grammatical parallelism and its Russian facet*. *Language and literature*, imehaririwa na Krystyna Pomorska na Stephen Rudy. Cambridge: Belknap Press.
- Jilala, H. (2016), *Misingi ya Fasihi Lingnishi. Nadharia Mbinu na Matumizi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company.
- Kahigi, K. K. (1995). Lugha Katika Vitabu Vya Watoto. Katika Kahigi K. K. (mh), Kioo cha Lugha: *Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi*. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juzuu, Na. 1. (uk. 21-36).
- Kezilahabi, E. (1976). *Ushairi wa Shaaban Robert*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Kiango, S. D. (1980). "Tamthiliya ya Kiswahili na Mabadiliko ya Dhamira 1957. 1975" Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kiango, S. D. (1982). "Tamthiliya ya Kiswahili: Dhamira Chapwa na Usuli katika Uchapwa". *Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi*. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Juzuu Na, 49/2 (uk: 33-56).
- King'ei, K. & Kisovi, C. (2005). *Misingi wa Fasihi Simulizi*, Nairobi: Literature Bureau.
- King'ei, K. (1987). "Usanifu wa Lugha katika Uandishi wa E. Hussein." Katika *Mulika Na. 19*. TUKI.
- Kombo, D. K. & Tromp, D. L. A, (2006). *Proposal and Thesis Writing: Introduction*, Nairobi: Paulines Publications Africa.

- Kothari, C. K. (1990). *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.
- Kothari, C. R. (1993). *Research Methodology: Methods and Techniques (Toleo la 2)*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.
- Kvale, S. (1996). *Interviews An Introduction to Qualitative Research Interviewing*. London: Sage Publications.
- Lakoff, G. & Johnson, M. (1980). *Metaphor We Live By*. Chicago: University of Chicago Press.
- Lakoff, G. & Johnson, M. (1988). *Metaphors we Live By (Toleo la 2.)*: Chicago: Chicago University Press.
- Lakoff, G. & Turner, M. (1989). *More Than Cool Reasons. A Field Guide to Poetic Metaphor*. Chicago: University of Chicago Press.
- Lanham, R. A. (1991). *A Handlist of Rhetorical Terms* London: University of California Press.
- Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. New York: Longman Group Inc. Limited.
- Mayoka, J. (1986). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mloka, Dae es Salaam*: TPH.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: EAEP.
- Mugenda, O. M. & Mugenda, A. G. (2003). *Research Methods: Qualitative and Quantitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.
- Mulokozi, M. & Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH.

- Mulokozi, M. M. & Kahigi, K. K. (1982). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*, Dar es Salaam: TPH.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: DUP.
- Mulokozi, M. M. (2012). *Korasi katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uhakiki*, TUKI.
- Mutembei, K. A. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K. & Chimera, R. M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Jomokenyatta Foundation. Tanzania.
- Nkwera, F. V. (1979). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyo*, Dar es Salaam: TPH.
- Oyoyo, J.O. (2013). *Tasnifu ya Uhakiki wa fani katika Ngano tano za Kiswahili*. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Padgett, D. (2002). *Qualitative Methods in Social Work Research*: Thousand Oaks: Sage Publications.
- Rashid, C. (2011). *Itikadi katika riwaya za Shaaban Robert*; Chuo kikuu cha Dar es Salaam.
- Sengo, T. S. Y. M. (2009). *Fasihi za kinchi, The registered trustees of AlAmin Education and Research Academy, Dar es Salaam*.
- TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. (Toleo la 2). Nairobi: Oxford University Press.
- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthiliya: Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publisher.

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa.



## VIAMBATISHO

### **KIAMBATISHI 1: Mwongozo wa Maswali kwa mtafiti**

Maswali yafuatayo yalitumiwa na mwanafasihi linganishi katika kuchambua diwani ya Ustadh Andanenga. Je, ni vipengele vipi vya mchomozo vimevyojitokeza katika diwani hii?

.....  
.....  
.....

1. Je, Vingepengele vya mchomozo vinafanana au vinatofautiana katika kazi hiyo ya ushairi
2. Ni kipengele kipi kilichotumiwa zaidi na mwandishi katika kuwasilisha maana ya matini yake?
3. Ni ipi dhima ya mwandishi katika kutumia vipengele vya mchomozo zinapotumiwa na mtunzi?